

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
3. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi - MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
5. Mhe. Haji Omar Kheri - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
6. Mhe. Haroun Ali Suleiman - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
7. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
8. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

9. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo - MBM/Waziri wa Afya/
Jimbo la Kiembesamaki
10. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu
na Mafunzo ya Amali /
Nafasi za Wanawake
11. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa
Biashara, Viwanda na
Masoko Zanzibar/ Uteuzi
wa Rais
12. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume - MBM/Waziri wa
Ujenzi, Mawasiliano na
Usafirishaji/ Uteuzi wa
Rais
13. Mhe. Rashid Ali Juma - MBM/Waziri wa Habari,
Utalii na Michezo/Jimbo
la Amani
14. Mhe. Hamad Rashid Mohamed - MBM/Waziri wa Kilimo,
Maliasili, Mifugo na
Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
15. Mhe. Maudline Cyrus Castico - MBM/Waziri wa
Uwezesaji, Wazee,
Vijana, Wanawake na
Watoto/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Salama Aboud Talib - MBM/Waziri wa Ardhi,
Maji, Nishati na
Mazingira/ Nafasi za
Wanawake
17. Mhe. Juma Ali Khatib - MBM/ Waziri Asiekuwa
na Wizara Maalum/ Uteuzi
wa Rais
18. Mhe. Said Soud Said - MBM/Waziri Asiekuwa
na Wizara Maalum/
Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Khamis Juma Mwalim - Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
20. Mhe. Harusi Said Suleiman - Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
21. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
22. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
23. Mhe. Chum Kombo Khamis - Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
24. Mhe. Lulu Msham Abdalla - Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Juma Makungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
26. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Jimbo la Mwanakwerekwe
27. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Jimbo la Jang'ombe
28. Mhe. Ali Khamis Bakar - Jimbo la Tumbe
29. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
30. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
31. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
32. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
33. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
34. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani

35. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
37. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
39. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
40. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
42. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
43. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
44. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
45. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
46. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
47. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
48. Mhe. Masoud Abraham Masoud	-	Jimbo la Bububu
49. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
50. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
51. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
52. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
53. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali-		Jimbo la Uzini
54. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
55. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
56. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
57. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
58. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Jimbo la Chukwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy-		Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake
Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kwanza - Tarehe 18 Mei, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

*(Wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kufunguliwa
kwa Mkutano wa Baraza)*

DUA

Mhe. Spika (*Zuberi Ali Maulid*) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba Mwenyezi Mungu atusaidie kuendesha shughuli zetu kwa amani na utulivu mkubwa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika naomba kuwasilisha Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 27 Juni, 2015.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Vile vile Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na za Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 49

Utekelezwaji Ahadi za Serikali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu na niwapongeze wale Waheshimiwa waliobahatika kukaa mstari wa mbele, na vile vile...

Mhe. Spika: Mheshimiwa tafadhali uliza swali.

Ahadi zinazotolewa katika Baraza la Wawakiishi na Mawaziri, wananchi huwa wanazisikia na Waziri anaetoa ahadi anapaswa kutekeleza ahadi yake kwa wakati.

- a) Ahadi zinazotelewa na Mawaziri hupitiwa mara ngapi kwa mwaka kujua ahadi gani zilitekelezwa na ambazo hazijatekelezwa kwa manufaa ya wananchi.
- b) Je ni hatua gani Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais huchukua pale Waziri ametoa ahadi kupitia chombo hiki na baadae kushindwa kutekelezwa na kero kubakia kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye kipengele (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. spika, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali huwa inafuatilia kwa karibu mijadala ya vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuratibu taarifa za utekelezaji wa Serikali, ikiwemo ahadi zinazotolewa na Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. spika, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi za kila mwaka wa fedha, ambazo pamoja na mambo mengine zinatoa maelezo ya utekelezaji wa malengo yaliyopangwa, ikiwemo ahadi zilizotolewa na Serikali kupitia Waziri husika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hukumbushia ahadi zinazotolewa na Mawaziri kwa kuandikia rasmi Wizara zao. Aidha Ofisi ya Baraza la Wawakilishi huchukua hatua kama hiyo kuziandikia Wizara kuhusu ahadi zinazotolewa na Waziri husika, kila baada ya Mkutanowa Baraza la Wawakilishi. Pia taarifa za utekelezaji zianzowasilishwa Serikalini huelezea ahadi mbali mbali zinazotolewa katika vikao vya Baraza la Wawakilishi. Vile vile Waheshimiwa Mawaziri hupata fursa kuzipitia mara nyingi ahadi hizo zilizotolewa katika taarifa mbali mbali zinazowasilishwa katika Baraza lako tukufu.

Kwa hivyo naamini Mhe. Spika, Waheshimiwa Mawaziri wanazielewa fika ahadi alizozitoa na wakati wote wanazitekeleza kwa ukamilifu.

- (b) Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais huwa inafuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa ahadi zinazotolewa kupitia sekta mbali mbali. Hivyo ni wajibu wa kila sekta husika kutekeleza ahadi zake ili kutimiza wajibu wake na Serikali huchukua hatua pale tu kosa linapotokea kulingana na kosa husika.

Kwa kiwango kikubwa Mhe. Spika, ahadi za Serikali zimetokelezw vizuri kupitia ilani ya uchaguzi ya mwaka 2010/2015 kwa ufanisi mkubwa wa zaidi ya asilimia tisini (90%) ahsante.

Mhe. Jaku Hassan Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza Suala moja la nyongeza.

- a) Mhe. Waziri ni ahadi ngapi zimetolewa ndani ya Baraza zinatakiwa kutekelezwa na muda gani na ngapi zimetokelezw na zipi bado hazijatelezwa hadi sasa.
- b) Serikali haioni kuna haja ya kuleta taarifa ya Baraza hili baada ya muda ili Wajumbe wajue Baraza hili na waweze kufahamu ahadi gani zimetokelezw na zipi hazijatekelezwa ikiwemo ahadi ya waandishi wa habari iandae chombo hiki. Chombo hiki hiki kimetangaza waandishi wa habari katika bajeti watalipwa wanaofanya kazi katika mazingira magumu

kwa chombo hiki, ahadi hiyo mpaka leo haijatekelezwa je, Serikali ahadi hiyo inatekeleza kwa mdomo kwa vitendo ikiwemo waandishi wa habari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wanapouliza swala wawe karibu na *mic* zetu hizi ili uweze kusikika vizuri hili swala, vyenginevyo inakuwa tabu kutokana na tatizo la *echo* la humu ndani na Mhe. Jaku analijua jambo hili kwa sababu ni mzoefu sana.

Mhe. Spika, kama ninavyosema kwamba ahadi zilizotolewa humu ndani ni nyingi sana na Ofisi yetu si rahisi kuweza kuratibu kila ahadi inayotolewa na Mhe. Waziri humu ndani, lakini kama nilivyosema anataka jibu la msingi kwamba kila Waziri anaratibu vizuri ahadi zake na anazitekeleza kama ambavyo ameahidi na pale panapotokea kasoro yoyote ya utekelezaji Baraza lako tukufu huarifiwa kwa ukamilifu wake.

Nataka niendeleo kumhakikishia Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wawakilishi wote pamoja na wananchi kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kutimiza ahadi zake zote ambazo imezitoa ndani ya Baraza na nje ya Baraza kwa ajili ya kuwatumikia vyema wananchi wa Zanzibar.

Kuhusu swala la Wafanyakazi wa Wizara ya Habari au waandishi wetu sikulisikia vizuri Mhe. Spika, ningeomba arudie tana.

Mhe. Jaku Hashim Ayob: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swala moja la nyongeza.

Serikali haioni kuna haja ya kuleta taarifa Barazani kila baada ya muda ili Wajumbe wa Baraza waweze kufahamu ahadi gani zimetekelezwa.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa Jaku alitaka ufafanuzi wa swali kipengele namba tatu cha swali lako kuhusu waandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayob: Chombo hiki *hansard* zipo, ahadi zipo waandishi wa habari ndio hawa tuliokuwa nao leo miaka miwili karibu hawajapata posho yao.

Mhe. Spika: Ni sawa....

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Lini watapata mwaka huu, mwakani, baada ya miaka miwili?

Mhe. Spika: Mheshimiwa hajafahamu swali lako la mwisho aliomba uliulize tena ili aweze kukujibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, bora angekaa akasikiliza.

Mhe. Spika: Mheshimiwa weka karibu *microphone*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Suala langu la pili la msingi, Serikali haioni kuna haja ya kuleta taarifa ndani ya Baraza hili baada ya muda ili wajumbe wajue kuna ahadi ngapi zimetokelezwa na ngapi hazijatekelezwa, ikiwemo ahadi ya Wajumbe kwa waandishi wa Habari wa ZBC ndani ya chombo hiki; muda mrefu wameahidiwa posho zao leo karibu mwaka wa pili wa tatu, ahadi hiyo imekuwa kwa mdomo tu kwa vitendo haitekelezeki. Sababu gani ya msingi ikawa haitekelezeki waandishi wa habari hawa, wakati wanafanya kazi kutoka kamati zetu katika chombo hiki hatuoni tunarudisha nyuma waandishi wa habari hawa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, lazima nirudie tena kusema kwamba tunapozungumza hapa tunajua matatizo yetu ya *echo*, kwa hivyo unaposema kwa haraka na jazba tunapata tabu sana kusikia maelezo ya Mheshimiwa Mjumbe. Na sisi kwa heshima kubwa tungependa kujibu kwa ufasaha maelezo ya Mhe. Muwakilishi.

Kwa msingi huo Mheshimiwa nataka niwahakikishie kwamba Serikali yetu kila aina ya ahadi ambayo imeitoa itatekelezwa kwa ukamilifu wake, na kama kuna jambo lolote ambalo lina malalamiko kwa ndugu zetu waandishi wa habari waliomo humu ndani ambao sikulisikia vizuri naomba Mheshimiwa aniandikie kwa maandishi tuweze kulishughulikia, kwa sababu inakuwa tatizo kumsikia anavyoeleza. Ni vizuri na yeye ni mwakilishi wa siku nyingi akaeleza kwa utaratibu tukaulewa kinachofanyika, ana uzoefu wa kutosha Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku hapana huwezi kuendelea.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, niliwahi kuwa muwakilishi kwa kipindi cha miaka kumi na tano nyuma na bahati nzuri uliwekwa utaratibu mzuri wa utekelezaji wa masuala na majibu katika Baraza. Mhe. Waziri wakati mwingine anakuwepo peke yake katika Baraza hili watendaji hawapo na huko ndio nakuhakikisha kunakwama kupata masahihisho mapema kwa ajili ya taarifa ya hayo masuala yanayokuja.

Je, utaratibu huo kwa sasa unazingatia vipi ili yanapoletwa masuala na Majibu Wizara fulani na watendaji wawepo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ni kawaida ya humu ndani ya Baraza wawakilishi mara nyingi Waziri anapokuja hapa watendaji hukaa juu kusikiliza majibu ya Mhe. Waziri, ili waweze kuyarikodi vizuri na aweze kuyaweka kumbukumbu kwa ajili ya utekelezaji. Lakini hata hivyo jibu lolote ambalo linahitaji utekelezaji Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais huchukua taarifa hizo na kumuandikia Waziri muhusika.

Vile vile kama nilivyosema katika jibu la msingi Baraza la Wawakilishi kupitia Katibu wa Baraza hufanya kazi hiyo ikiwasilisha rasmi kwa Wizara husika kwa ajili ya utekelezaji. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba kila kazi ambayo inapaswa kutekelezwa na Serikali itafanyika ipasavyo na kuwatumikia wananchi kwa uadilifu mkubwa.

Nam. 10

Tatizo la Upatikanaji wa Ajira Kwa Vijana Wenye Elimu Ndogo

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:

Mhe. Spika, zinatangazwa nafasi za ajira Serikalini zinakuwa na masharti magumu wakati kazi nyengine hata vijana waliomaliza *Form III* wanaweza kufanya.

- a) Je, Serikali haioni kuwa vijana hawa nao wana haki ya kufanya kazi kwa sababu kazi nyengine hazihitaji elimu kubwa, zinahitaji hekima na busara na utulivu wa mtu.
- b) Je Serikali ina mpango gani wakusaidia wasomi wenye elimu ndogo kupata ajira hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vipengele (a) na (b), lakini kwanza naomba kutoa maelezo mafupi.

Mhe. Spika, utaratibu wa ajira katika Taasisi za Umma umeelezwa wazi katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011, kifungu cha 58(2) na 59(1) kuwa, fursa za ajira zitazingatia kiwango cha elimu na sifa kulingana na nafasi ya kazi inayohitajika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba vijana wetu wenye kiwango kidogo cha elimu, wana haki ya kufanya kazi hasa kwa nafasi za kazi ambazo sifa za kuajiriwa hazihitaji kuwa na elimu ya juu. Ili kulitekeleza suala hili, Serikali imekuwa ikizingatia fursa za ajira kulingana na mahitaji ya Taasisi husika. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya vijana 166 wenye kiwango cha elimu ya sekondari wameajiriwa katika Taasisi za Umma katika ngazi mbali mbali za kiutawala na uendeshaji.
- (b) Mhe. Spika, Serikali imeandaa Mipango kadhaa ya kuwasaidia vijana wenye elimu ya sekondari kupata ajira. Miongoni mwa mipango hiyo ni kuwajengea uwezo vijana hao ili waweze kuajiriwa au kujiajiri, ikiwa pamoja na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na mikopo ili waweze kujiajiri wenyewe. Mpango huu kwa sasa unatekelezwa na Wizara inayoshughulikia masuala ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, fursa hiyo ya mafunzo ya Ujasiriamali na mikopo inategemea utayari wa kijana mwenyewe kuweza kujiunga na mafunzo hayo kwa shughuli anayotaka kuifanya. Vijana wenye elimu ya Kidato cha pili, tatu na nne ni miongoni mwa vijana wanaoweza kufaidika na fursa hiyo. Hivyo napenda kutoa wito kwa vijana kuitumia fursa hii ipasavyo. Aidha naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwahamasisha vijana wetu wajitokeze kutumia fursa zilizopo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.

Spika, ni kweli kwamba serikali hupokea maombi tofauti kutoka kwa vijana wetu ambao wanahangaika kutafuta ajira, lakini maombi yanapokuja serikalini na ambapo fursa zinakuwa hazipo au hazitoshi. Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako inajipangaje kuwasaidia hawa vijana kuwaunganisha na ajira ambazo zitakuwepo huko nje katika sekta binafsi.

Je, wizara yako itakuwa ipo tayari kwa kusaidiana pamoja na Wizara ya Kazi kuanzisha *job centres* ambapo vijana wanaweza kwenda kwenye halmashauri zetu kujiorodhesha na pale fursa zinapotokea wanaweza kufaidika na kusaidiwa kwa pamoja. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, Wizara yetu ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi kama ulivyozungumza itakuwa tayari kushirikiana na wizara hiyo katika suala zima la kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira ikiwa ndani ya nchi au nje ya nchi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri ameeleza kuwa utaratibu wa ajira umeelezwa katika sheria ya ajira ya utumishi wa umma, nilitaka kujua je utungwaji wa kanuni za sheria ile umefikia wapi hadi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, suala la utayarishaji wa kanuni tayari limeshakamilika.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri taratibu za serikalini mwisho ni miaka 60 kufanya kazi, lakini sasa hivi kuna watu wanaozidi miaka 60 katika taasisi mbali mbali za serikali na wakati kuna vijana wenye sifa za elimu na hawana ajira. Je, nilikuwa napenda kujua vijana hawa wataajiriwa lini. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, ni kweli kama ulivyozungumza baadhi ya wafanyakazi wanakuwa na umri huo wa miaka 60, lakini kwa kuwa sheria na utaratibu wa kuongezewa muda ipo na inafanya kazi inakuwa haki hiyo inapatikana pale iwapo watakuwa wanahitaji kufanya hivyo.

Nam. 5

Ujenzi wa Uwanja wa *Mao Tse Tung*

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Serikali ya SMZ chini ya Kiongozi imara Dkt. Ali Mohammed Shein inastahiki pongezi kwa kuamua kuujenga upya Uwanja wa Mao lakini mbali na maamuzi hayo mazuri.

- a) Je, ujenzi wa uwanja huo utanza lini na kumalizika lini.
- b) Je, gharama ya ujenzi wa uwanja huo utakuwa kiasi gani hadi kumalizika kwake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye kipengele (a) na (b), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein imeamua kuujenga Uwanja wa *Mao Tse Tung*.

Mhe. Spika, mkataba wa awali tayari umeshatiwa saina na serikali na vile vile mkataba wa utekelezaji wa mradi huo umeshasainiwa na serikali tarehe 28/4/2016. Hivyo basi, kilichobakia sasa ni kusubiri tu uanzaji wa ujenzi huo ambapo ndugu zetu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wapo katika maandalizi ya kukamilisha tararibu za mwisho za kuanza kwa ujenzi huo.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

- (a) Ujenzi wa Uwanja wa *Mao Tse Tung* unatarajiwa kuanza kabla ya tarehe 20 mwezi wa Disemba mwaka huu, hii ni kwa mujibu wa mkataba wa utekelezaji uliosainiwa tarehe 28 April, 2016 kati ya Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Mhe. Spika, ujenzi huu unatarajiwa kuchukua miezi kumi na tatu. Hivyo basi, ni matumiani yetu utakapokamilika mwanzoni mwa mwaka 2018.

- (b) Mhe. Spika, kuhusu gharama za ujenzi wa uwanja huo zinatarajiwa kufikia jumla ya wastani wa Tshs.10,000,000,000/- ambazo watatoa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na jumla ya Tshs. 600,000,000/- zitachangiwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Spika, mbali na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamua kwa mapenzi ya wananchi wake na wana michezo wake kujenga upya uwanja huu wa *Mao Tse Tung*.

Mhe. Spika, uwanja wa *Mao Tse Tung* ulikuwa na viwanja viwili; uwanja mkubwa na uwanja ule mdogo wa pili.

- a) Je, katika ujenzi huu utajengwa ukiwa viwanja viwili au kimoja.
- b) Mhe. Spika, pili niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya China kwa vile Serikali ya Watu wa China katika ushirikiano mkubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar na mapenzi makubwa ya Watanzania imeamua kwa asilimia kubwa kutujengea uwanja ule. Je, serikali ina mpango gani kuishawishi tena wapenzi wetu na washirika wetu hawa wa Serikali ya China kujenga viwanja vyengine kila Mikoa kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli nakiri kwamba vile viwanja vilikuwa viwili na tayari vimeshawekewa usafi kwa ajili ya ujenzi huo, nakuahidi kwamba hiki kiwanja kitakuwa cha aina yake kwani kitajengwa kimoja na cha kimataifa. Pia utakuwa ni shahidi kwa kuwa umo katika jimbo hili la Kikwajuni utauona huu uwanja kama ni wa aina yake.

Mhe. Spika, nakubali kwamba kuna kila sababu ya kuwashauri ndugu zetu wa Kenya kushirikiana na ndugu zetu wapenzi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kutujengea viwanja vyengine. Hili nikuahidi kwamba serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kuna mpango wa kujenga viwanja vyengine kila Wilaya. Nakuahidi kwamba wana michezo wetu wote hakuna sababu ya kuwa wasishiriki katika michezo ya mipira na michezo mingineyo. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, asante naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Je, amejandaa vipi na

kujipanga kuhusu masuala ya ajira kwa wazalendo katika masuala ya hoteli pamoja na *restaurant za standard* ya juu pamoja na za chini, kwa sababu hizi ajira nyingi katika mahoteli wanapata Wakenya wanaambiwa Wazanzibari...

Mhe. Spika: Mheshimiwa samahani swali la msingi linahusiana na uwanja wa *Mao Tse Tung* kwa vile maswali ya nyongeza yalenge hapo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana basi nitakaa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri uliyoeleza katika swali lako mama naomba nimuulize Mhe. Naibu je, ni sababu gani ambazo zilichelewesha ujenzi wa uwanja huo mpaka kufikia muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba huu ujenzi ulichelewa nakiri, lakini hii inatokana na sababu kwa kuwa huku kuna utaratibu wa mikataba baina ya ma-*contractor* na serikali. Kwa hiyo, hii tumeamua kwa makusudi kwamba tusiweze kukurupuka kwa kuchagua mtu tu, kwa sababu ameleta *tender* pengine ana mtu amemtumilia kuwa anatarajia asilimia kumi. Kwa hiyo, hii tumefanya hivi kwa makusudi ili tuchague wakuleta *tender* ili kupata *contractors* wazuri kwa kujenga kiwanja chenye hadhi na sifa nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika jibu la msingi alisema serikali iko tayari kujenga viwanja vyenye uhadhi na ubora katika kila Mikoa. Je, serikali kwa sasa ilikuwa na mpango wa kutia *tartan* katika uwanja wa Gombani Pemba, ni sababu zipi zilizosababisha mpaka leo *tartan* ile hajajengwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli uwanja wa Gombani umechelewa kutiwa *tartan* lakini sababu iliyosababisha kuchelewa kwa uwanja ule ilikuwa ni udhaifu wa mkandarasi ambaye alipewa kazi ile, na kwa umahiri wa wizara na ufuatiliaji uliofanywa na serikali baada ya kutoridhika na hali ambayo ilifikiwa katika uwanja wa Gombani, ilionekana ni busara serikali isitishie taratibu ile na itafute mtu ambaye anaweza kufanya kazi kwa makini na kama ipasavyo. (*Makofi*)

Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika ufatiliaji huo tayari zana zote za kutia *tartan* ya kukimbilia uwanja wa Gombani zimefika. Kazi hiyo tayari inatarajiwa kukamilika punde tu si zaidi ya mwezi wa sita baada ya kumfukuza yule ambaye alitia *tartan* kwa kiwango ambacho hakikubaliki. Kwa hivyo, mheshimiwa asiwe na wasi wasi uwanja wa Gombani muda mfupi unaweza ukatumika katika njia ya *tartan*. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 15

Kupatiwa Elimu kwa Vikundi vya Ujasiriamali

Mhe. Bahati Khamis Kombo – Aliuliza:-

Wanawake wengi sasa hivi wameamka kujiajiri wenyewe pamoja na kujiunga katika vikundi mbali mbali zikiwemo *SACCOS* na vikoba lakini vikundi hivi baadhi ya shehia vinakufa haraka kwa kukosa elimu ya ujasiriamali.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kuviboresha vikundi hivi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshimwia kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi na wasaa huu kufika siku ya leo.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15.

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na ukweli kuwa, vikundi vingi vya miradi vinavyoanzishwa huwa vinakufa baada ya muda mfupi. Hali iko sio kwa Zanzibar pekee, bali utafiti umethibitisha hali hiyo ipo kwenye nchi nyingi zinazoendelea. Kuna sababu nyingi zinazochangia kufa kwa vikundi na miradi hiyo, na moja wapo ni ukosefu wa taaluma za ujasiriamali.

Mhe. Spika, sababu nyengine ni uzoefu mdogo wa wanavikundi hao juu ya uendeshaji na uongozi wa vikundi hivyo, pamoja na taaluma duni ya usimamizi wa fedha na upatikanaji wa huduma za kuimarisha biashara (*Business Development Service – BDS*).

Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo wizara yangu ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inatekeleza mpango kabambe wa kuviwezesha vikundi vya wajasiriamali na vyama vya ushirika vikiwemo vya akiba na mikopo (SACCOS), ili kuimarisha utendaji wao na kujipatia tija kama ifuatavyo:

Wizara kwa kupitia programu ya miundombinu ya masoko, kuongeza thamani za mazao na huduma za fedha vijijini, imetoa mafunzo kwa viongozi 1,152, wanawake 728 na wanaume 424 kwa SACCOS na vyama vya ushirika vya uzalishaji.

Wizara imetoa mafunzo kwa wanachama 6,588 juu ya haki na wajibu wao kubadili mitazamo na uimarishaji wawekezaji wa akiba.

Wizara imetoa mafunzo kwa wajasiria mali 639, wanawake wakiwa ni 572 na wanaume 67 kupitia kituo chake cha kulelea, kukuza wajasiriamali kilichopo chuo cha Karume, Mbweni ambacho kwa jina jengine kinaitwa *incubator*. Mafunzo hayo yalijumuisha vikundi 17 vya wajasiriamali kama kampuni. Pia wizara inaendelea na mpango wa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wanaochukua mikopo kabla ya kukopeshwa, mikopo hiyo kutoka Mfuko wa Uwezeshaji wa wanachama kiuchumi uliopo katika wizara. Jumla ya vikundi 143 na wajasiriamali mmoja mmoja 419 walipewa mafunzo hayo.

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji wa mipango hiyo bado asasi zisizo rasmi kama vile vikoba na vile ambavyo havijajitokeza na kusajiliwa rasmi bado havijafaidika na mipango hii. Kwa hivyo, nawashauri wananchi kupitia vikundi vya asasi wajitokeze na waje kwa mashauriano ili tuweze kuona jinsi tutakavyoweza kuwahudumia kupitia programu zinazoendeshwa na wizara yangu.

Mhe. Spika: Mhe. Bahati Khamis Kombo naona ameridhika na swali naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kama lilivyotangulia swali la msingi kwamba vikundi vingi vya SACCOS na Vikoba vinakufa na katika tatizo hili ndani ya Jimbo langu la Magomeni kuna SACCOS ya Magomeni ambayo nasema imekufa na mimi nilikuwa ni mwanachama.

Swali langu ni kwamba, pamoja na kuendelea kufa kwa vikundi hivi kikiwemo kikundi cha Magomeni, wizara yake inachukua hatua gani ya kuweza kuhakikisha kwamba vikundi hivi havifi au vilivyokufa vinafufuka. Kwa sababu vikundi ambavyo vinakufa wakati mwingine tayari wananchi ambao walikuwa ni wanachama wamekuwa na madeni wanadai. Je, Mhe. Waziri atakuwa na hatua gani juu ya suala hili ambapo vikundi hivi viko chini ya wizara yake.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa ikiwa na yeye ni mmoja wapo wa kikundi hicho kwamba wizara yangu inatambua jambo hili na imefuatilia ndio maana imeweza kutoa takwimu hizi ili kuhakikisha kwamba vimepatikana na vipo ili tuvifuatilie. Lakini jambo ambalo nimeligundua langu binafsi kwa uzoefu wa ujasiriamali ni pamoja na kuwapa watu mikopo halafu hawafuatiwi wakasaidiwa kwa ukaribu. Kwa hiyo, wengine wanabadilisha matumizi ya awali wanatumia kwa mambo mengine.

Kwa hiyo, napenda kukuhakikishia Mheshimiwa kwamba ofisi yangu itajipanga rasmi kuhakikisha kwamba vikundi vyote vilivyokuwa na matatizo viweze kufundishwa ipasavyo na ikiwezekana kuwashajiisha kwa mara nyengine kuwawezesha ili waweze kuendelea vizuri.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba pamoja na utelekezaji wa mipango hiyo asasi zisizo rasmi kama vile vikoba havijafaidika na mipango hiyo. Je, wizara ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba vikundi hivi vya vikoba au asasi hizi vinafaidika na mipango hii ili kuwasaidia hususan kinamama kufaidika na mipango hii.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama Mheshimiwa anenisikiliza vizuri ni pale niliposema kuna hawa ambao hawajafaidika na vikoba vilivyoko kwenye wizara ni vile ambavyo vimejitegemea. Kwa makusudi nimetoa wito hapa rasmi kwa wale wote ambao vikoba vyao havijasajiliwa rasmi kwenye wizara yetu waje tuonane nao, tuwashauri kwa kupitia ushirika tujue ni jinsi gani tunaweza tukawapanga katika maeneo yetu ili waweze kufaidika na mpango maalum wa mikopo inayotoka kwenye wizara yangu. (*Makofi*)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Nichukue nafasi hii pia kuipongeza sana serikali kwa kujitahidi sana kuwapa mafunzo wajasiriamali wetu. Mhe.

Naibu Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba tatizo kubwa la wajasiriamali wetu ni kutokuwa na taaluma, lakini pia amesema anafahamu kwamba pamoja na tatizo hilo kubwa alilolizungumza la ukosefu wa taaluma pia wajasiriamali wetu wana tatizo kubwa la ukosefu wa soko.

Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wajasiriamali wetu wanasaidiwa kupata soko la nje na ndani ya nchi.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kwamba wizara kutokana na tatizo kama hilo ndio maana imeanzisha sehemu maalum ya kuwafundisha huko Mbweni ambayo inaitwa *incubator*. Mheshimiwa wanaingizwa pale kama ni watu ambao ni vifaranga vidogo hawana taaluma yoyote na kama wanayo taaluma ya kiasi fulani basi wanasaidiwa kuelimishwa ili wakitoka pale watoke na ujuzi mzuri, hatuwaruhusu kutoka pale mpaka wawe na uwezo wa kuweza kutengeneza bidhaa zao zitakazoweza kuuzika.

Wanapewa mafunzo yote mpaka *process* ya *finishing* na kuhakikisha kwamba tunawasaidia kwenda kwenye masoko. Mpaka sasa hivi wamekuwa na masoko mengi sana ambao wengine kwenye mahoteli yote wanauza sabuni, mishumaa ambayo ina harufu mbali mbali kutokana na mazao tunayolima Zanzibar ikiwa pamoja na karafuu, mdalasini na mengine mengi ambayo yapo Zanzibar.

Pia wengine wamepata masoko hata Marekani ni namna gani tu jinsi ambavyo wamejipanga wamesaidia kwenye *finishing*. Lakini pia tumewasaidia sana kuhakikisha kwamba kila kipindi cha sherehe ya Saba Saba, Nane Nane ya biashara Dar es Salaam wana vikundi hao wanachukuliwa rasmi kwenda kuangalia, kuona na kujifunza na pia kuchukua anuani mbali mbali kwa ajili ya huduma hiyo na wamepata huduma kiasi cha kusema kwamba mpaka sasa hivi uzalishaji walionao vijana hawa walioko pale wamekuwa hawana bidhaa ya kutosha.

Vile vile kuna wengine wanatengeneza maziwa ambayo wamekwenda kwenye mahoteli *demand* imekuwa ni kubwa kuliko *supply*. Kwa hiyo, utaona kwamba wizara iko katika kufanya jitihada ya kuhakikisha masoko yanapatikana. Lakini pia natoa wito kwa wawakilishi wote kabla hawajatoka katika kipindi hiki wapate nafasi ya kutembelea maeneo yetu ambayo tunaonesha biashara na shughuli zinazofanyika kuanzia wiki hii wakipata nafasi wakati wa *break* mchana nawaomba sana wapite pale Mbweni katika kituo hiki, wakaangalie wenyewe bidhaa na shughuli zinazofanyika pale. Inawezekena ikawa wao ni wanunuzi wa mwanzo. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 1

Matatizo ya Maji Jimbo la Kijitoupele

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibiwa swali langu Nam. 1 lakini lina marekebisho kidogo. Marekebisho ya Kwarara kwa Madina, hakuna Kwarara kwa Madina ni Kwarara/Madina isomeke hivyo.

Tatizo la maji katika Jimbo la Kijitoupele ni kero kubwa kwa wananchi katika baadhi ya maeneo kama vile Kwarara, Kwarara kwa Madina, Taveta, Tomondo Uzi, Meli nne, pamoja na meli Nne Uzi.

Kwa kuwa tatizo hilo lipo kwa muda mrefu sasa je, wizara yake ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa maeneo hayo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa waziri pamoja na marekebisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi pamoja na marekebisho yake swali lake Nam. 1 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa baadhi ya maeneo ya Jimbo la Kijitoupele yanakabiliwa na tatizo la upungufu wa huduma ya maji safi na salama. Hii inatokana na kukua kwa mahitaji ya maji ndani ya eneo hilo.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari inaendelea na juhudi za kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo kwa kuchimba visima katika maeneo ya Kwarara/Madina, Tomondo, Uwanja wa Magirisi, Kijito Upele na Fuoni Ijtimai kupitia mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras-al-Kheimah. Kukamilika kwa mradi huo kutaweza kutatua tatizo linalowakabili wananchi wa Kijitoupele.

Mhe. Spika, hivyo wizara yangu inamuomba Mhe. Mwakilishi na wananchi wa eneo hilo kuwa wastahamilivu wakati jitihada za kulipatia ufumbuzi tatizo hilo linaloendelea, lakini pia kutoa wito kwake na wananchi kutoa mashirikiano yao katika uendelezaji wa visima hivyo. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Kijitoupele ambalo limeanzia Kwerekwe Nyumba mbili hadi Meli Tano Nyumba Moja mpaka Kwarara na kwengineko, lakini kwa bahati mbaya au nzuri Mhe. Shamsi Vuai Nahodha alipokuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe pamoja na Mbunge wake Mhe. Haji Juma Serewaji walichimba kisima kikubwa sana Meli Tano Kijitoupele.

Lengo lake hivi sasa jimbo la Kijitoupele nachukulia lote liwe halina shida ya maji hata sehemu moja, kwa bahati nzuri Mamlaka ya Maji inatumia maji hayo kwa manufaa yao kwa kuuza kila siku katika magari. Wananchi wa maeneo haya ya Taveta, Meli Nne/Uzi, Meli Nne yenyewe, Kijitoupele *Dispensary* mpaka huko Kwarara ninakosema na Tomondo/Uzi hawapati maji, maji yake ya kudowea kwa muda maalum.

Namuuliza Mhe. Naibu Waziri je, kwa kuwa maji yale lengo lake kuwanufaisha wananchi wengi kuliko wizara kupata maji kwa manufaa yao Mamlaka ya Maji ina mpango gani wa kuliondoa tatizo hilo la kuwaungia watu maji katika maeneo hayo ili wafaidike wananchi wa jimbo langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza serikali haina azma ya kuwapa maji baadhi ya watu tu, ina azma ya kuwapa maji wananchi wote ndio maana kama alinisikiliza vizuri katika swali la msingi nilisema kwamba tayari vimechimbwa visima Kijitoupele kwenye hiki kisima cha kawaida nyuma yake, Tomondo Maduka saba na sehemu nyengine ambazo nimezitaja kwa lengo la kuondosha kabisa tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Sasa ukamilikaji wa visima hivi kutaondoa tatizo sio hapo tu Jimbo la Kijitoupele lakini pia na maeneo mengine *Inshaallah*.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji pia lipo katika Jimbo langu la Fuoni na visima vingi vinavyotoa huduma ya maji hivi sasa vimo katika jimbo hilo, lakini baadhi ya maeneo hawapati maji. Je, ni lini wananchi wangu wa maeneo ya Fuoni Birikani, Kiembeni na Ijitimai watapata hiyo huduma ya maji safi na salama. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, katika mpango wa uchimbaji wa visima moja kati ya jimbo ambalo limefaidika na uchimbaji huo ni jimbo lake na yeye atakuwa shuhuda kama atazunguka

kwenye jimbo atagundua kwamba visima vingapi tayari vimechimbwa. Mwenyezi Mungu akitujaalia sio muda mrefu hili tatizo litatataka.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Serikali imekuwa na uchimbaji wa visima vingi sana katika maeneo mbali mbali ili kuweza kutatua tatizo la maji, lakini tatizo hilo limekuwa likiendelea siku hadi siku katika maeneo mbali mbali.

Je, wizara yake ina mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa maji mbadala ili wananchi waweze kufaidika na maji na waweze kuepukana na tatizo la maji la kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli kwamba visima vimekuwa vingi na tunaendelea kuvichimba kwa sababu tunapambana na tatizo la uhaba wa maji. Hii kama nilivyosema mwanzo kwamba miji inakua na kadiri inavyokua mahitaji ya maji yanaongezeka. Sasa usitegemee kwamba kuna siku itakuwa halipo moja kwa moja lakini litapungua kwa sababu miundombinu imepita hapa, lakini kesho mwananchi anajenga pale na anahitaji maji, kwa hiyo itabidi huduma wapelekewe. Serikali inahakikisha kwamba haichoki kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata maji safi na salama.

Pia hivi visima ambavyo tayari vimechimbwa na kwa faida yako havipungui 150 tunataka vifanyiwe *connection* ya kwamba viwe vinapeleka maji kwa wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba. Ahsante sana.

Nam. 13

Wakulima Kupatiwa Zana za Kilimo za Kisasa

Mhe. Bahati Khamis Kombo – Aliuliza:-

Kilimo ndio uti wa mgongo na wananchi wengi hivi sasa wamekuwa na muamko wa kulima lakini wanalima kwa mazoea tu ukilinganisha nguvu zinazotumika na wanachovuna.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwapatia wakulima hao matrekta na pembejeo za kutosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika ahsante sana, kwanza awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuamka salama. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo naomba kumfahamisha kwamba, matumizi ya pembejeo za kilimo hasa mbegu bora, mbolea na zana za kilimo za kisasa ni nyenzo muhimu zinazosaidia katika kuongeza tija na mavuno kwa zao la mpunga. Aidha, napenda nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa kutambua kwamba kilimo ndio uti wa mgongo na nakubaliana naye kuwa wananchi wengi hivi sasa wamekuwa na muamko wa kulima, lakini wanalima kwa mazoea tu ukilinganisha nguvu zinazotumika na wanachovuna ni kidogo.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufahamu umuhimu wa matumizi ya pembejeo na hali duni za wakulima kupitia iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili ilianzisha programu ya kutoa ruzuku kwa wakulima wa mpunga wa kisasa cha asilimia 80 na wakulima wanachangia asilimia 20.

Kuanzia mwaka wa fedha programu hii ni ya miaka mitano 2011-2012 na 2015-2016. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itaendelea na utoaji wa ruzuku hiyo kwa kila msimu na kadri hali itakavyoruhusu.

Aidha, Wizara imepanga kuufanyia mapitio mpango wa utoaji wa ruzuku kwa ajili ya kwa ajili ya kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza na kuimarisha mpango huo. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Bahati ameridhika Mhe. Omar Seif Abeid swali la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kunipa nafasi hii asubuhi hii kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, kwa sababu zao la karafuu ndio kianzio kikubwa cha pato la taifa na kwa sababu mikarafuu mingi imeanza kuzeeka na wananchi wameonesha muamko wa kupanda mikarafuu mipya. Swali lipo hapa. Je, Wizara hii

ikishirikiana na Shirika la Biashara la Taifa la ZSTC lina mpango gani la kuwawezesha wakulima wa karafuu kuweza kuliendeleza zao hilo ili kukuza kipato cha mkulima na pato la taifa. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba angerejea swali na sio maelezo.

Mhe. Spika: Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, swali langu lipo kwa wakulima wa karafuu. Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia kuwawezesha wakulima wa zao la karafuu.

Mhe. Spika: Uliza swali la msingi mheshimiwa ulilouliza kuhusiana na wakulima wa karafuu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Sawa Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Swali tu, yaani uliza lile swali. Maelezo tumeshayasikia mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika. Basi Mhe. Spika, naomba kuondoa swali. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Basi nitampa kwanza Mhe. Jaku Hashim Ayoub halafu atafuatia Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, Programu ya miaka mitano ya kutoa ruzuku kwa wakulima ni asilimia 80 aliyosema hapa. Je, ni tija gani kwa wakulima ambayo mpaka sasa uwezeshaji bado unaonekana umeshuka soko la mahitaji ya mchele yanayotoka Tanzania Bara, ninafikiri hajanisikia naomba nirudie tena Mhe. Spika.

Programu ya miaka mitano ya ruzuku kwa wakulima ni asilimia 80. Je, imeleta tija gani kwa wakulima ambao mpaka sasa uwezeshaji wao bado unaonekana umeshindwa kutumia soko la ndani la mahitaji ya mchele na kubaki kutumia upatikanaji wa mchele kutoka Tanzania. Hilo ni la kwanza.

La pili, ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali moja tu kwa sababu hukuuliza swali la msingi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam!

Mhe. Spika: Ndio, swali moja tu, tuendelee Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Uaratibu Mhe. Spika, swali la nyongeza yanakuwa mawili.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, swali lake sijui kama nimemfahamu sahihi, anataka kujua labda sijui hawa wakulima kakusudia sijui wakulima wa juu....

Mhe. Spika: Wamenufaikaje na hiyo programu ya miaka mitano.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ninapenda kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa wakulima wamefaidika kutokana na kulimo cha umwagiliaji maji kutoka magunia waliyokuwa wakulima machache na kupata magunia mengi zaidi. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi).

Mhe. Simai Mohammed Saidi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri niseme tu kwamba ninakumbuka katika hotuba, alipokuja kuzindua Baraza letu rasmi hapa Mhe. Rais; Mhe. Waziri wa Wizara husika mchango wake ulikuwa nzuri sana.

Swali langu ni kwamba kama swali la msingi lilivyosema kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na kilimo ni hatua; kuwa unalima, unapanda, unavuna halafu unatafuta masoko kwenda kuuza hayo mazao yako.

Swali langu ni je, Mhe. Naibu Waziri baada ya hawa wakulima wote kuwapatia haya matrekta, pembejeo na mengine. Je, Wizara yako ipo tayari kujenga masoko kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu. Kwa mfano Unguja Ukuu Kae-Bona, Dunga Mitini, Mahonda, Kivunge ili tuweze kuwaunganisha wakulima wetu na masoko yote yaliyokuwepo huko ya mahoteli na utalii kwa ujumla. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Simai kwa kupitia swali lako. Wizara husika kwa kushirikana na Wizara ya Fedha itajenga masoko hayo. Na kwa sasa hivi ninafikiri tayari mchoro wa jengo la soko umeshakamilika, lile la kule Malindi. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Swali la mwisho la nyongeza. Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri ametwambia kutokana na programu hii ni kwamba kuna ongezeko kubwa sana la tija. Ningeomba atutajie idadi ya *tons* ya juzi na mwaka jana.

Kwa hivyo ninataka idadi za *tons* ambazo zimepatikana.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe naomba utupe, msaidie.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa kazi nzuri aliyioifanya.

Pili naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

Kwanza Mhe. Spika, mahitaji ya mchele yanayotoka nje ya nchi hapa ni *tons* 80,000 na mahitaji si chini hekta 15,000 ili uweze kuzalisha mpunga wa kuweza kuzalisha kupata kiasi hicho kinachoagiziwa kutoka nje.

Katika *tons* hekta 8,500 zilizopo ni hekta 800 tu ndizo zinazomwagiliwa maji hivi sasa na katika hekta 800 zinazomwagiliwa maji ni asilimi 40 tu ndiyo miradi yake inafanya kazi sawa sawa. Kwa hivyo, kwanza tuna safari ndefu ya kuweza kukamilisha mapato halisi ya kuzuia uletaji wa mchele kutoka nje ya nchi.

La pili, wakulima wameboreshwa sana. Mwanzo walikuwa wakipata kama gunia mbili, sasa hivi wanapata 0.9 kwa hekta za uzalishaji hivi sasa. Mategemeo yetu katika programu mpya tunayoanza nayo sasa hivi baada ya kuzungumza na ndugu zetu kutoka Israel, watafanya *drips irrigation* na tunategemea wakulima wetu wataanza kuzalisha kwa kiwango kikubwa zaidi na kuweza kuzitumia hizi hekta 8,500 zilizopo ili tuweze kujitosheleza kwa mchele.

Vile vile tuna mpango wa hekta 34,000 zilizopo juu za kutega maji ya mvua na zenyewe vile vile tutaingia kwenye programu ili tuhakikishe katika kipindi cha miaka mitano hii, suala la kuagizia chakula liwe limemalizika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri swali lilikuwa la kitakwimu na majibu yametoka mazuri tu, ninashukuru. Waheshimiwa Wajumbe mpaka hapa itakuwa tumefikia mwisho wa sehemu ya maswali. Sasa naomba nimwite Katibu kwa shughuli inayoendelea, Katibu.

Mhe. Waziri kabla hujasoma hiyo taarifa naomba nitoe taarifa ya wageni tulionao, halafu utaendelea.

Waheshimiwa Wajumbe wageni tulionao ni wageni wa Mhe. Simai Mohammed Said ni viongozi wa CCM kutoka Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na viongozi wa Jimbo la Tunguu. Jumla wao ni watu 8, wanaongozwa na Ndg. Ramadhan Abdalla Ali ambaye ni Mwenyekiti wa CCM katika Mkoa wa Kusini Unguja na Mwenyekiti wa CCM Jimbo la Tunguu Ndg. Khatib Ramadhan Iddi. (*Makofi*)

Pamoja na wao, naomba na wale wengine wasimame ili Waheshimiwa waweze kukuoneni.

Ahsanteni wale pale.

Taarifa yangu ya mwisho nimeipata kutoka kwa Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei) amepata msiba wa shangazi yake. Kwa hivyo, amenitaka nikujuulisheni hilo na pamoja na taarifa kwamba yeye atakuwa amekwenda Pemba kwa ajili ya shughuli hiyo. Ahsanteni.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango naomba uendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17. Sambamba na Hotuba hii, naomba kuwasilisha vitabu viwili. Kitabu cha Kwanza cha Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2015 na cha Pili ni Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17. Taarifa zote hizo zimezingatia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, Mkakati Mpya wa Maendeleo wa Zanzibar 2016-2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoitowa kwenye uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba nitangulize Hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, ikiwa ni pamoja na sisi waja wake. Namshukuru kwa kutupa uhai, afya na uwezo na kukutana tena katika shughuli hii muhimu katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu nchi yetu na wananchi wake. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie sote hekima na busara katika mijadala ya kikao hiki, atujaalie heri, baraka na maelewano kati yetu. Atupe pia utulivu, upendo na mshikamano miongoni mwetu. Bila ya yeye, hatuna nguvu wala uwezo wa kufanya lolote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa moyo wa dhati naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa ushindi wa kishindo aliyoupata katika Uchaguzi wa Mwaka 2015 na kwa kuanzisha mageuzi makubwa ya utawala kwa faida ya wananchi walio wengi chini ya kauli mbiu ya HAPA KAZI TU!!!!. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu naomba pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed kwa Ushindi wa Kishindo aliyoupata katika Uchaguzi wa Marudio wa mwezi Machi 2016. Hii inaonesha kuwa wananchi wengi wana imani sana na Rais wetu Mpendwa. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais ambaye pia ni

Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa uongozi makini wa nchi yetu. Hekma, busara na jitihada zake zimeendelea kuiweka Zanzibar katika utulivu na amani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, aidha, nachukua fursa hii pia kumpongeza Msaidizi Mkuu wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa ushauri wake na kufanya kazi kwa karibu zaidi na Mheshimiwa Rais. Kutokana na umakini wa Kiongozi wetu huyu nchi yetu inanza awamu ya pili ya kipindi cha miaka mitano ya awamu ya saba tukiwa na utulivu mkubwa. Halikadhalika, kutokana na umakini wake kwa Mhe. Rais, nchi imezidi kupiga hatua kimaendeleo kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo. Naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango kwa uadilifu na uoni wao na miongozo wanayotupatia katika utayarishaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango na Uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sasa nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zuberi Ali Maulid kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo kuwa Spika wa Baraza letu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2016-2020). Nakutakia heri na mafanikio katika kuendesha na kusimamia vyema vikao vya Baraza letu lenye sura mpya. Tunaamini hayo hayatowezekana bila ya ushirikiano madhubuti, hekma na busara za wasaidizi wako wote akiwemo Mhe. Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Sheha Hamad Mattar Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hekima, busara na uoni wenu vitasaidia sana katika kuishauri Serikali na kuifanya iwajibike vyema zaidi kwa wananchi wake. Hapana shaka kazi yenu kubwa ya kuliendesha Baraza kwa njia ya kidemokrasia na uwazi itawezesha kuliongoza vizuri na kwa umakini mkubwa.

Mhe. Spika, aidha, kwa nafasi ya kipekee naishukuru Kamati ya Wenyeviti ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyo chini ya Uongozi wa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo na vile vile Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, Makamu wa Mwenyekiti wake na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa maoni na ushauri waliotupatia. Nakiri kuwa mumetusaidia kuifanya taarifa hii ninayoiwasilisha hapa kuwa bora zaidi yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo chanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili ama kwa kuchaguliwa na wananchi katika Majimbo yao au

kupata uteuzi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa wajumbe wa Baraza hili. Ni imani yangu kuwa wajumbe sote tutapokea imani hii ya wananchi na ya Mheshimiwa Rais kwa kuchapa kazi kwa bidii, uadilifu na uaminifu mkubwa ili kuiletea nchi yetu maendeleo ya haraka.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani yake kubwa kwangu na kuamua kuiteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Dhima niliyonayo kwake na kwa wananchi wa Zanzibar ni kutekeleza majukumu yangu kwa umakini mkubwa na kwa maslahi ya Taifa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, niruhusu pia kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Donge kwa kunipa imani yao ya kunichagua kuwa Mwakilishi wa jimbo lao kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na nawaambia kwamba sitowaangusha. Vile vile naishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono na kunisaidia kufanikisha majukumu yangu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, hotuba yangu ya leo imegawika katika sehemu kuu mbili. Kwanza ni Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2015/16 na pili ni Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17.

Mhe. Spika, ili tupate maendeleo endelevu ya jamii yetu, tunahitaji uchumi wetu ukue vyema kila mwaka na kuwanufaisha wananchi walio wengi. Tunashukuru kwamba kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 uchumi wetu ulikua kwa kiwango cha kuridhisha cha wastani wa asilimia 7. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa sekta ya viwanda, huduma, kilimo, uvuvi na misitu, sekta ndogo za ujenzi, fedha na bima, usafiri, habari na mawasiliano na utawala wa umma. Kwa upande wa Pato la mtu mmoja mmoja, pia limeendelea kuongezeka kutoka TZS 1,065,000 (USD 683) kwa mwaka 2011 kufikia TZS 1,632,000 (USD 817) mwaka 2015.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2015

Hali ya Uchumi Duniani

Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Spika, uchumi wa dunia kwa mwaka 2015 umeendelea kukua ingawa kasi ya ukuaji wake imepungua kidogo na kufikia wastani wa asilimia 3.1

ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 kwa mwaka 2014, ukiathiriwa zaidi na mwenendo katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea. Uchumi wa nchi zilizoendelea umekua kwa wastani wa asilimia 1.9 kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 1.8 kwa mwaka 2014. Kasi ya ukuaji imepungua katika nchi zinazoibukia na zinazoendelea ambapo uchumi wake umekua kwa wastani wa asilimia 4.0 kwa mwaka 2015 kutoka asilimia 4.6 mwaka 2014.

Hali kama hiyo ya kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi imejitokeza katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambako ukuaji umeshuka hadi asilimia 3.4 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2014. Vile vile, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Kanda ya Afrika Mashariki imepungua kidogo kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2014 kufikia asilimia 5.9 mwaka 2015.

Mwenendo wa Mfumko wa Bei Duniani

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2015 imepungua na kufikia asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.5 mwaka 2014. Upungufu huo umejitokeza katika nchi zilizoendelea, ambako kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2015 imepungua hadi asilimia 0.3 kutoka asilimia 1.4 mwaka 2014. Hata hivyo, kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi mfumko wa bei ulibakia kuwa na kasi ile ile ya wastani wa asilimia 4.7. Kuendelea kushuka kwa bei za bidhaa za chakula, mafuta na gesi asilia kumesaidia kuleta hali hiyo ya utulivu wa bei.

Mhe. Spika, licha ya kushuka kwa bei za bidhaa za chakula na mafuta katika soko la dunia kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imeonekana kupanda kutoka asilimia 6.4 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2015, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yaliosababisha ukame na kupungua kwa uzalishaji wa ndani.

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kushuka kidogo na kufikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2014. Kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Afrika ya Mashariki kumetokana na kushuka kwa bei za mafuta na chakula duniani pamoja na kuongezeka uzalishaji wa ndani.

Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar Ukuaji wa Pato la Taifa

Mhe. Spika, Uchumi wa Zanzibar bado unaendelea kuimarika. Kwa mwaka 2015, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2007 lilikua kwa wastani wa

asilimia 6.6. Kiwango hicho cha ukuaji kipo juu ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.0 kwa nchi zinazoendelea na asilimia 3.4 kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, kasi hiyo inaashiria kupungua kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2014.

Mhe. Spika, ukuaji huu wa Pato la Taifa umechangiwa na mambo yafuatayo:

i) Kuimarika kwa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2015, kutoka upungufu wa asilimia 0.4 mwaka 2014. Hali hii imesababishwa na ukuaji mzuri katika Sekta ndogo za Uvuvi (8.2%), Mifugo (7.5%) na Misitu (4.0%). Hata hivyo, Sekta ndogo ya mazao imeendelea kupungua ambapo kwa mwaka 2015 ilipungua kwa asilimia 1.6.

ii) Kuimarika kwa Sekta ya Viwanda ambayo imekua kwa wastani wa asilimia 10.6 mwaka 2015 kutoka ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2014. Shughuli ambazo zilikuwa kwa kasi ni Ujenzi asilimia 12.5, Uchimbaji Mawe na Mchanga asilimia 10.9, uzalishaji viwandani asilimia 8.9, umeme na gesi asilimia 6.7 na usambazaji wa maji safi na salama na uondoshaji wa maji machafu asilimia 5.7.

iii) Pia kukua kwa pato la Taifa ulichangiwa na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sekta ya huduma imeendelea kukua kwa kasi baada ya kukua kwa asilimia 8.0, na kutanguliwa tu na sekta kuu ya viwanda. Hata hivyo, kasi hiyo ya ukuaji wa asilimia 8.0 inamaanisha kupungua kwa ukuaji kwani mwaka 2014 kasi ya ukuaji ilifikia asilimia 9.8. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa sekta ndogo ya habari na mawasiliano kutoka asilimia 24.7 mwaka 2014 hadi asilimia 7.7 mwaka 2015, kupungua kwa shughuli za sekta ndogo ya biashara na ukarabati kutoka asilimia 13.0 mwaka 2014 kufikia asilimia 1.2 mwaka 2015 na kupungua kwa sekta ndogo ya taaluma, sayansi na ufundi kutoka asilimia 43.4 mwaka 2014 kufikia asilimia 15.0 mwaka 2015.

Mhe. Spika, hata hivyo, ukuaji wa sekta ndogo kadhaa umekuwa mzuri na kufikia tarakimu mbili, ikiwemo malazi na chakula (10.2), huduma za fedha na bima (11.2), huduma za taaluma, sayansi na ufundi (15.0), Utawala (12.9), Utawala wa Umma (13.3), Sanaa na uburudishaji (17.2) na huduma nyenginezo (14.7).

Pato la Mwananchi

Mhe. Spika, Ukuaji huo wa uchumi wetu umepelekea pato halisi la Taifa kwa mwaka 2015 kufikia TZS 2,308 bilioni kutoka TZS 2,133.5 bilioni mwaka 2014. Kasi kubwa ya ongezeko la pato la Taifa kuliko ya ongezeko la idadi ya watu kimepelekea kuongezeka kwa wastani wa pato la Taifa la kila mtu kufikia TZS 1,632,000 mwaka 2015 kutoka TZS 1,552,000 mwaka 2014 kwa bei za miaka husika. Kushuka kwa sarafu ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani kwa wastani wa asilimia 20.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014 kumepelekea thamani ya pato la mtu binafsi kwa dola kupungua kutoka wastani wa dola 939 hadi dola 817 kwa mwaka 2015. Hata hivyo, kwa kutumia bei za kudumu za mwaka 2007 bado wastani wa Pato la mtu binafsi limeongezeka kutoka dola 651 mwaka 2014 hadi dola za Marekani 674 mwaka 2015.

Mchango wa Sekta mbali mbali katika Pato la Taifa

Sekta ya Kilimo

Mhe. Spika, kuimarika kwa sekta ya huduma na sekta ya Viwanda kumeshusha mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa kwa mwaka 2015 na kufikia wastani wa asilimia 19.2 kutoka asilimia 27.9 mwaka 2014. Aidha, ukiacha sekta ndogo ya mifugo ambayo imeendelea kuchangia asilimia 2.8 ya pato la Taifa, mchango wa sekta ndogo zote za kilimo umeshuka ikilinganishwa na mwaka 2014. Mchango wa sekta ndogo ya mazao umefikia wastani wa asilimia 9.1 mwaka 2015 kutoka asilimia 15.9 mwaka 2014. Sekta ndogo ya uvuvi imechangia asilimia 4.9 mwaka 2015 kutoka asilimia 6.4 mwaka 2014, sekta ndogo ya misitu imechangia asilimia 2.4 mwaka 2015 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2014.

Sekta ya Viwanda

Mhe. Spika, utafiti wa kijamii na uchumi wa mwaka 2015 unaonesha kuimarika kwa sekta ya viwanda, kwa kasi kubwa zaidi ya ukuaji na mchango wake kwa uchumi wetu. Mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 19.8 mwaka 2015 kutoka asilimia 16.8 mwaka 2014. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda kumetokana na kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya ujenzi na kufikia wastani wa asilimia 9.5 mwaka 2015 kutoka asilimia 7.9 mwaka 2014, sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kufikia wastani wa asilimia 8.0 mwaka 2015

kutoka asilimia 6.4 mwaka 2014 na sekta ndogo ya uchimbaji mawe na mchanga kufikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2015 kutoka asilimia 1.5 mwaka 2014.

Mchango wa sekta ndogo ya umeme na gesi kwa mwaka 2015 umeendelea kubaki asilimia 0.3. Hata hivyo, mchango wa sekta ndogo ya maji safi na huduma za michirizi ulipungua na kufikia asilimia 0.4 mwaka 2015 kutoka asilimia 0.8 mwaka 2014.

Sekta ya huduma

Mhe. Spika, kama ilivyotarajiwa katika dira ya maendeleo ya 2020, sekta ya huduma imeendelea kuwa muhimili mkuu wa uchumi wetu. Kwa mwaka 2015, mchango wa sekta ya huduma katika pato la Taifa umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 49.1 kutoka asilimia 44.7 mwaka 2014. Kuongezeka huko kumetokana na kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya utawala wa umma uliofikia asilimia 10.9 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2014, sekta ndogo ya taasisi za fedha na bima kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2015 kutoka asilimia 4.1 mwaka 2014 na usafirishaji na uhifadhi uliofikia asilimia 5.2 mwaka 2015 kutoka asilimia 4.0 mwaka 2014.

Vile vile, mchango wa sekta ndogo ya elimu uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2015 kutoka asilimia 2.0 mwaka 2014. Hata hivyo, mchango wa sekta ndogo ya habari na mawasiliano ulipungua na kufikia asilimia 3.5 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2014 na sekta ndogo ya huduma za malazi ulifikia asilimia 8.1 mwaka 2015 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2014.

Mfumko wa Bei

Mhe. Spika, utulivu wa bei za bidhaa na huduma ni chachu muhimu ya maendeleo ya kiuchumi. Kasi ya mfumko wa bei kwa bidhaa na huduma imefikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2014. Hali hiyo ya kupanda kidogo kwa kasi ya mfumko wa bei nchini, imesababishwa na kupanda kwa mfumko wa bei za bidhaa za chakula kutoka asilimia 4.4 mwaka 2014 hadi asilimia 7.4 mwaka 2015.

Mwenendo huo wa bei za chakula uliathiri mwenendo mzuri uliojitokeza katika bei za bidhaa zisizo za chakula, ambazo kasi yake ya mfumko wa bei ilipungua kutoka asilimia 6.8 hadi asilimia 4.0 katika kipindi hicho, kukichangiwa na kushuka kwa bei za bidhaa za mafuta ikiwemo dizeli, petroli na mafuta ya taa.

SEKTA YA NJE

Biashara na Nchi za Nje

Mhe. Spika, kwa mwaka 2015 mwenendo wa biashara na nchi za nje umeonesha matokeo mchanganyiko. Kwa upande mmoja, nakisi katika urari wa biashara na nchi za nje imepungua kwa asilimia 21.5 kutoka nakisi ya TZS 145.9 bilioni mwaka 2014 hadi nakisi ya TZS 114.5 bilioni mwaka 2015.

Mhe. Spika, kwa upande mwingine, shughuli za biashara zimeonekana kupungua mwaka 2015 ikilinganishwa na 2014. Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi ilipungua hadi TZS 42.4 bilioni mwaka 2015 kutoka TZS 133.6 bilioni mwaka 2014 sawa na punguzo la asilimia 68. Kupungua kwa thamani ya usafirishaji kumetokana na kupungua kwa usafirishaji wa mazao ya biashara kama vile karafuu na mwani. Jumla ya tani 1,463 zenye thamani ya TZS 24.8 bilioni za karafuu zilisafirishwa mwaka 2015 ikilinganishwa na tani 2,777 zenye thamani ya TZS 50.8 bilioni kwa mwaka 2014. Aidha, tani 8,073 tu za mwani zenye thamani ya TZS 5.9 bilioni zilisafirishwa mwaka 2015 chini ya kiwango cha tani 13,806 zenye thamani ya TZS 8.5 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2014.

Mhe. Spika, uagizaji wa bidhaa kutoka nje nao umepungua na kufikia TZS 156.9 bilioni mwaka 2015 kutoka TZS 279.6 bilioni mwaka 2014. Karibu maeneo yote ya uagizaji yameonesha kupungua mwaka 2015 ikilinganishwa na mwaka 2014. Upunguaji huo unajitokeza zaidi katika uingizaji wa magari, vifaa vya umeme na vifaa vya ujenzi.

Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Mhe. Spika, tofauti na taswira ya biashara ya nje, biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara imeimarika zaidi mwaka 2015. Uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umefikia thamani ya TZS 73.8 bilioni mwaka 2015 kutoka thamani ya TZS 64.3 bilioni mwaka 2014. Aidha, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umefikia TZS 401.2 bilioni mwaka 2015 kutoka ya TZS 366.3 bilioni mwaka 2014.

Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kuwa miongoni mwa sekta muhimu katika uchumi wa Zanzibar kutokana na uwekezaji, ajira, uhusiano wake na sekta nyengine na kuwa chanzo muhimu cha mapato ya Serikali. Kwa mwaka

2015 idadi ya watalii walioingia nchini ilifikia 294,243 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 5.7 ikilinganishwa na watalii 311,891 walioingia nchini mwaka 2014. Kupungua kwa idadi ya uingiaji watalii nchini kumechangiwa na mripuko wa kesi za maradhi ya Ebola katika nchi za Afrika ya Magharibi yanayotajwa kupunguza idadi ya watalii kwa Bara la Afrika kwa asilimia 6, hali ya kiuchumi kwa baadhi ya Nchi za Ulaya na mwaka 2015 kuwa mwaka wa Uchaguzi Mkuu nchini.

Hata hivyo, Zanzibar imeanza kupokea Mashirika mapya ya ndege zinazowasili moja kwa moja nchini. Aidha, imeanza pia kupokea watalii kutoka masoko mapya katika nchi za Poland, China, Israel, Urusi na India ambao kwa ujumla, wameongezeka kwa asilimia 31.5 kutoka watalii 22,106 mwaka 2014 hadi 29,070 mwaka 2015.

UKUZAJI RASILIMALI

Mhe. Spika, thamani ya ukuzaji rasilimali imeongezeka kwa asilimia 3.3 kufikia TZS 588.8 bilioni mwaka 2015 kutoka TZS 570.1 bilioni mwaka 2014. Hii imetokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika shughuli za ujenzi, kutoka TZS 371.4 bilioni mwaka 2014 na kufikia thamani ya TZS 429.8 bilioni mwaka 2015.

Vile vile, kuongezeka kwa shughuli za mifugo kufikia TZS 4.7 bilioni mwaka 2015 kutoka TZS 4.1 bilioni mwaka 2014 na ongezeko la vifaa mbali mbali kufikia TZS 17.8 bilioni mwaka 2015 kutoka TZS 15.6 bilioni mwaka 2014. Hata hivyo, thamani ya uwekezaji wa vifaa vya usafirishaji imepungua kutoka TZS 79.1 bilioni mwaka 2014 hadi TZS 47.9 bilioni kwa mwaka 2015 sawa na upungufu wa asilimia 39.4 na vifaa vyenginevyo kutoka TZS 99.8 bilioni mwaka 2014 hadi TZS 88.4 bilioni mwaka 2015 sawa na upungufu wa asilimia 11.4.

UWEKEZAJI BINAFSI

Mhe. Spika, idadi ya miradi iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), imeongezeka kutoka miradi 26 yenye thamani ya dola za Kimarekani 526.7 milioni mwaka 2014 hadi miradi 32 yenye thamani ya dola za Kimarekani 318.1 milioni mwaka 2015 sawa na punguzo la thamani kwa asilimia 39.6. Idadi ya ajira mpya zimeongezeka kwa mwaka 2015 kutoka ajira 1,084 mwaka 2014 hadi ajira 1,515. Kupungua kwa uwekezaji binafsi kwa mwaka 2015 kunatokana na msimu mdogo wa uwekezaji. Vile vile, imetokana

na kupungua kwa uwekezaji katika sekta ndogo ya hoteli na mikahawa. Hata hivyo, uwekezaji katika sekta ndogo ya ujenzi wa nyumba za kukodi na shughuli za biashara umeongezeka maradufu.

SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki

Mhe. Spika, Huduma za kibenki ni moja wapo ya sekta za kiuchumi ambazo zimekuwa zikiimarika kwa kasi katika kipindi cha hivi karibuni. Hadi kufikia Machi 2016 Amana za benki zimeongezeka kwa asilimia 33.8 na kufikia TZS 718.3 bilioni kutoka TZS 536.8 bilioni katika kipindi kama hiki mwaka 2015. Hali hii ilichangiwa na uhamasishaji wa benki kutokana na ushindani ukiambatana na kuimarika kwa huduma za kibenki kupitia simu za mikononi. Mikopo katika benki iliongezeka kwa asilimia 77.3 na kufikia TZS 358.6 bilioni hadi Machi mwaka 2016 ikilinganishwa na TZS 202.3 bilioni zilizotolewa kipindi kama hiki mwaka 2015. Uwiano wa mikopo na amana uliongezeka kutoka asilimia 37.7 hadi asilimia 49.9.

Mhe. Spika, Kati ya mikopo ya TZS 358.6 bilioni iliyotolewa, mikopo katika miradi binafsi ilifikia asilimia 45.2, utalii asilimia 23.4, biashara asilimia 15.9, ujenzi asilimia 4.3 na mawasiliano na usafirishaji asilimia 2.3. Sekta zilizobakia kwa ujumla zilipokea mikopo ya asilimia 8.4 iliyobakia.

THAMANI YA FEDHA YA TANZANIA

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2015, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 20.8 ikilinganishwa na kushuka kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Kwa mwaka 2015 Dola moja ya Kimarekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 1,997 ikilinganishwa na wastani wa TZS 1,653 mwaka 2014. Hali hii imetokana na kuimarika kwa Dola ya Marekani dhidi ya Sarafu nyengine, bei ndogo ya mazao ya asili yanayosafirishwa nje, na kupungua kwa mapato mengine kutoka nje, ikiwemo misaada na mikopo. Kulijitokeza pia tatizo la benki na wafanyabiashara kuhodhi fedha za kigeni katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2015/2016 Serikali ilikadiriwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya TZS 450.5 bilioni sawa na asilimia 19.5 ya Pato la Taifa. Matumizi yalikadiriwa kuwa TZS 830.4 bilioni sawa na asilimia 35.9 ya Pato la

Taifa. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2015 hadi Machi 2016, mapato ya ndani yalifikia TZS 306.1 bilioni sawa na asilimia 90 ya makadirio. Maelezo zaidi juu ya utekelezaji wa Bajeti nitayatoa baadae katika Hotuba yangu ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/17.

MAENDELEO YA KIUCHUMI

Mhe. Spika, Kuendelea kukua kwa uchumi wa Zanzibar kumekwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

- i) Kuongezeka kwa idadi ya wateja wapya waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa kutoka 10,440 mwaka 2014 hadi 12,366 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 18.4.
- ii) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za msingi za Serikali na binafsi kutoka 252,938 mwaka 2014 hadi kufikia 261,212 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 3.1.
- iii) Kuimarika kwa utoaji wa huduma katika sekta ya afya kwa kuongezeka kwa madaktari kufikia 155 mwaka 2015 kutoka madaktari 148 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 4.7, wauguzi kufikia 1,089 mwaka 2015 kutoka wauguzi 1,026 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 6.1 na kuongezeka kwa watabibu (*clinical officers*) kwa asilimia 14.3 kutoka watabibu 189 mwaka 2014 kufikia 216 mwaka 2015.
- iv) Kuongezeka kwa matumizi ya simu na mtandao kutoka idadi ya laini 1,337,361 mwaka 2015 ikilinganishwa na laini 1,155,478 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 15.7.
- v) Kuongezeka kwa wanafunzi waliopatiwa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 2,823 mwaka 2013/14 hadi kufikia wanafunzi 3,499 mwaka 2014/15 sawa na ongezeko la asilimia 24.
- vi) Kuongezeka kwa zahanati kutoka 53 mwaka 2014 kufikia zahanati 67 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 26.4.

- vii) Kuongezeka kwa visima vilivyochimbwa kwa ajili ya huduma ya usambazaji maji, kutoka visima 28 vinavyozalisha mita za ujazo 15,120 kwa siku kwa mwaka 2014 hadi visima 74 vilivyozalisha mita za ujazo 44,380 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 164.
- viii) Kuendelea kudhibiti maradhi ya malaria kwa kuongezeka kwa upulizaji wa dawa majumbani kufikia nyumba 64,156 mwaka 2015 kutoka nyumba 34,140 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 87.9.

MASUALA MTAMBUKA

i) Programu ya Tuzungumze na Watoto (T-Watoto)

Mhe. Spika, Programu hii inalenga kuelimisha jamii na watoto juu ya kuimarisha hali na ustawi wa kimaisha kwa Wazanzibari katika masuala mbali mbali kama maji, elimu, afya, usafi wa mazingira na kadhalika. Kupitia programu hii tafiti mbili zimefanyika; ya kwanza ilihusiana na masuala ya maji na usafi wa mazingira (*Water, Sanitation and Hygiene - WASH*) na ya pili ilihusiana na sekta ya elimu hususan maandalizi na msingi.

Mhe. Spika, Tafiti ya *WASH* ililenga zaidi kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia maji safi na salama kwa matumizi ya kijamii katika familia ili kuepukana na maradhi. Baadhi ya matokeo ya msingi ya utafiti huo ni kwamba asilimia 90.6 ya wanafamilia wanapata maji kutoka kwenye vyanzo vilivyoimarishwa kwa matumizi ya majumbani; asilimia 85.7 ya wanafamilia nyumba zao zina vyoo na asilimia 48.9 wanaondoa taka ngumu majumbani kwa kuchoma moto na asilimia 10.3 wanatupa baharini au mtoni.

Mhe. Spika, kwa upande wa elimu, Programu imekusudia kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa elimu ya maandalizi na msingi ambazo ndio nguzo za matokeo mazuri kwa watoto katika elimu ya sekondari, vyuo na upatikanaji rasilimali watu iliyo bora hapo baadae. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wanafamilia wamekubali ulazima wa elimu kwa watoto wao na kwamba akina mama wanaongoza kwa kutumia muda mwingi zaidi kuzungumza na watoto wao juu ya masuala ya elimu.

Mhe. Spika, Kamati Tendaji ya Utekelezaji wa tafiti hizi hivi sasa inaendelea na mchakato wa uandaaji wa utafiti wa tatu juu ya athari za Maradhi ya Kipindupindu (*Cholera*) kwa watoto na jamii kwa jumla.

ii) Utekelezaji wa Program ya Mafuta na Gesi na Matamasha ya Ajira kwa Vijana Zanzibar

Mhe. Spika, Katika kuendeleza fursa za ajira kwa vijana, Serikali kwa kushirikiana na kampuni ya Mafuta ya *SHELL* imetekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo kuwajengewa uwezo walimu katika vyuo mbali mbali vya Amali nchini kuendana na mahitaji ya soko; Kamati maalum ya Vijana na Ajira kwa Taasisi binafsi (*Zanzi - Job Committee*) imeundwa; Programu ndogo ndogo ya “*world of work*” na programu ya “*recruit-me*” inayomilikiwa na Kampuni ya Simu ya *TIGO* zimeanzishwa pamoja na kuimarishwa kwa Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira ili vijana waweze kujisajili.

Mhe. Spika, Kati ya mwaka 2014 na 2015 Matamasha mawili ya Ajira kwa Vijana yalifanyika Unguja na Pemba. Tamasha la tatu limefanyika tarehe 30 Aprili, 2016 ambapo vijana wasio na ajira zaidi ya 500 na Makampuni zaidi ya 30 walishiriki. Matamasha haya yanawakutanisha pamoja waajiri/makampuni na vijana kwa dhamira ya kurahisisha upatikanaji wa ajira ambapo vijana 44 wameweza kuajiriwa au kujiajiri kupitia matamasha hayo.

iii) Uimarishaji wa Taarifa za Msingi za Wilaya

Mhe. Spika, Katika mwaka 2008, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (*UNICEF*) iliandaa Taarifa za Msingi za Wilaya (*District Profiles*) kwa madhumuni ya kuwa na chanzo cha uhakika cha taarifa za msingi kwa wilaya zote za Zanzibar ili zitumike katika kupanga mipango mbali mbali ya Maendeleo kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa. Taarifa hizi za msingi za Wilaya zinahusisha Takwimu za Elimu, Afya, Maji, Idadi ya watu na mgawanyo wake kiumri na kijinsia, ardhi, kilimo, mifugo, misitu, uvuvi, ulemavu, vitega uchumi, masuala ya hali ya hewa, miundombinu, mazingira na kadhalika.

Mhe. Spika, Kwa sasa taarifa hizo ni za muda mrefu na zinahitaji kufanyiwa mapitio. Ni matarajio ya Serikali kwamba mapitio hayo yatakapokamilika yatawezesha kuwepo kwa taarifa na takwimu zenye kuendana na wakati zitakazopelekea kuandaliwa mipango yenye kuzingatia vigezo vya mahitaji halisi. Hivyo, natoa wito kwa watendaji wa Wilaya zote kuendelea kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Kamati na maafisa wanaotekeleza zoezi hili la mapitio ili kufikia lengo lililokusudiwa.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO 2015/2016

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/16 ulipanga kutekeleza jumla ya programu 28 na miradi 37 ya maendeleo kupitia Klasta tatu za *MKUZA II*. Kati ya hizo, programu tatu zenye jumla ya miradi sita zinatokana na Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*) unaojumuisha Programu Mjumuisho ya Kuimarisha Utalii; Programu ya Mazingira Bora ya Biashara na Programu ya Utafutaji Rasilimali Fedha. Kwa mwaka 2015/16, programu na miradi ya maendeleo ilipangiwa jumla ya TZS 398.9 bilioni.

Kati ya fedha hizo, TZS 51.9 bilioni zilitarajiwa kutolewa na Serikali kutokana na mapato ya ndani sawa na asilimia 13.0 na TZS 347.1 bilioni zilitarajiwa kutoka nje kupitia kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 87 ya bajeti yote. Jumla ya TZS 98.2 bilioni ni ruzuku na TZS 248.9 bilioni ni mkopo.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2015/16, programu na miradi mbali mbali iliyotarajiwa kupata fedha nyingi haikuweza kuanza au kusitishwa utekelezaji kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kutokamilika kwa taratibu za mikataba na manunuzi. Miradi hiyo ni pamoja na Uendelezaji wa ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume lililokadiriwa TZS 146.5 bilioni; ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja TZS 7.9 bilioni, Ujenzi wa barabara tatu za Jendele – Cheju – Unguja Ukuu Kaebona, Kizimbani – Kiboje na Jumbi – Koani zenye jumla ya TZS 12.0 bilioni; Programu ya umwagiliaji TZS 26.5 bilioni na mradi wa Uwekaji Kamera na Vifaa vya Ulinzi TZS 10.0 bilioni.

Mhe. Spika, Kufuatia hali hiyo kufikia Machi 2016, jumla ya TZS 67.9 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 17.0 ya Bajeti ya Maendeleo. TZS 14.6 bilioni zilitolewa na Serikali sawa na asilimia 28.1 na TZS 53.3 bilioni sawa na asilimia 15.3 zilitolewa na Washirika wa Maendeleo. Upatikanaji wa kiwango hiki cha fedha kwa miezi tisa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ni pungufu kwa TZS 49.4 bilioni ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa 2014/15.

Mhe. Spika, Serikali imeendelea kutekeleza azma ya kupunguza wingi wa miradi ili kuleta ufanisi wa utekelezaji. Jumla ya miradi saba inapendekezwa kukamilika kutegemea na upatikanaji wa fedha baina ya April na Juni 2016. Jumla ya TZS 4.5 bilioni zinahitajika kukamilisha Programu na miradi hiyo ambayo ni:

- i) Programu ya Utafiti wa Kilimo na Maliasili;
- ii) Mradi wa kuimarisha Mikarafuu;
- iii) Mradi wa Ujenzi wa barabara za Jendele/Cheju/Unguja Ukuu Kaebona;
- iv) Mradi wa Uimarishaji wa Kiwanja cha ndege cha Pemba kwa uwekaji wa taa za kuongozea ndege;
- v) Mradi wa Ujenzi wa uzio/Ukuta wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume;
- vi) Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu;
- vii) Mradi wa *Barefoot* Awamu ya Kwanza

UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika, Serikali katika mwaka 2015/16 iliendelea na juhudi za kukuza uchumi kwa kufanya mageuzi ya kiuchumi na ya Serikali ili kufikia malengo ya *MKUZA II* na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020. Mkazo uliwekwa katika utekelezaji wa maeneo yafuatayo: Mpango wa Matokeo kwa Ustawi; Kuimarisha huduma za kijamii; kuendeleza sekta ya nishati, kutekeleza programu za kukuza ajira kwa vijana, kuendeleza uvuvi wa bahari kuu pamoja na kuendelea kuvutia wawekezaji kwa sekta za viwanda. Utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*)

Mhe. Spika, Mpango wa Matokeo kwa Ustawi, (*R4P*) unajumuisha programu tatu; nazo ni Programu Mjumuisho ya Kuimarisha Utalii; Programu ya Mazingira Bora ya Biashara na Programu ya Utafutaji Rasilimali Fedha. Shughuli zilizofanywa kupitia Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii ni pamoja na uwekaji wa Taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege Pemba, kutayarisha ramani na *BOQ* kwa kituo kimoja cha utoaji taarifa za usalama kwa watalii chenye vyumba viwili. Mchakato wa kuandaa mfumo wa kisasa wa upatikanaji wa soko kwa kutumia mtandao umeanza unaotegemewa kuwa na lugha tano za kimataifa.

Mhe. Spika, Kwa upande wa Programu ya Mazingira Bora ya Biashara shughuli mbali mbali zimetokelezwa zikiwemo kuandaliwa kwa Rasimu ya Mapendekezo ya Sera ya Maendeleo ya Wajasiriamali, kuanzishwa kwa Vituo vya kutoa huduma kwa wajasiriamali katika maeneo ya vitamizi (*clusters*) vya *TEHAMA* na ukarabati wa jengo la Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni na ununuzi wa samani.

Mhe. Spika, Katika Programu ya Kuimarisha Upatikanaji wa Rasilimali Fedha, uchunguzi wa hesabu kwa mashirika sita ya Serikali na marekebisho ya Sheria ya Wakfu yamefanyika. Aidha, rasimu ya awali ya Kanuni ya uanzishwaji na usimamizi wa mashine za kutolea risiti (*EFD*) imetayarishwa pamoja na Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 yamefanyika.

Mhe. Spika, Katika eneo la kuimarisha Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi, mafunzo juu ya dhana, Sera na Sheria ya Mashirikiano ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi yametolewa kwa Makatibu Tawala wa Miko na Wilaya zote za Unguja na Pemba na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Maofisa wa *PPP* wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi Tanzania Bara. Vile vile, mafunzo kwa mfumo wa moduli yametolewa na wataalamu kutoka Benki ya dunia ambayo yamewashirikisha wafanyakazi 56 kutoka katika Taasisi za Serikali. Jumla ya miradi 10 ya awali imeteuliwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na hatua za kumtafuta mtaalamu elekezi zimeanza.

Kuimarisha Huduma za Kijamii

Mhe. Spika, Huduma za kijamii za elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama zimeimarishwa kwa kuondosha michango kwa skuli za Msingi na Maandalizi, kuifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Abdalla Mzee kwa ujenzi wa majengo ya ofisi, kutolea huduma za dharura, kutolea huduma za matibabu ya nje, kufanyia matengenezo ya vifaa tiba pamoja na vyumba vya upasuaji vinne. Aidha, ununuzi wa dawa muhimu kwa ajili ya hospitali na vituo vyote vya afya Unguja na Pemba umefanyika.

Mhe. Spika, Kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini na vijijini, ujenzi wa magari umefanyika katika maeneo ya Matemwe, Ndagoni, Vikunguni, Taifu, Mtemani, Chake Mjini na Mkoani. Aidha, kazi ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa vibanda vya kuendeshea mitambo umefanyika katika maeneo mbali mbali sambamba na kazi ya kufunga pampu pamoja na upelekaji umeme vituoni. Jumla ya visima 148 kati ya 150 tayari vimeshachimbwa na kati ya hivyo visima 10 vimeendelezwa.

Kuendeleza Sekta ya Nishati

Mhe. Spika, Kuhusu Kuendeleza Sekta ya Nishati maafisa wa ngazi mbali mbali wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo yanayohusiana na masuala ya Mafuta na Gesi ndani na nje ya nchi. Serikali tayari imeandaa Sera ya Mafuta na Gesi na kwa sasa inaendelea na maandalizi ya Sheria.

Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu

Mhe. Spika, Katika kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na umeme imeanza kwa ajili ya ujenzi wa Diko na soko jipya la samaki Malindi. Hata hivyo, ujenzi huo haujaanza kutokana na changamoto mbali mbali zikiwemo kuchelewa kukubaliana na *UNESCO* juu ya matakwa ya uhifadhi wa Mji Mkongwe. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza Novemba, 2016. Kwa upande wa Uvuvi wa kina kirefu cha maji, wavuvi 45 kwa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo. Kampuni ya Hairu ya Sri Lanka imetiliana saina makubaliano ya awali ya kuanzisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kuendeleza miradi mikakati ya Uwekezaji

Mhe. Spika, Katika utekelezaji na uendelezaji wa miradi mikakati ya uwekezaji, miundombinu imeimarishwa katika maeneo huru ikiwemo kuanzisha Mpango wa Fumba *Bay Satellite City*. Shughuli za Mpango Mkuu wa Fumba zimeendelezwa katika hatua ya kusimamia kazi ya upasuaji wa njia kuu tatu - Fumba.

Mhe. Spika, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni mama ya "Bakhressa *Group of Companies*" imeajiri Makampuni ya *Phills International* ya Dubai kukamilisha mpango mkuu wa mradi wa Mji wa Biashara Fumba (*Fumba Satellite City*). Viwanda viwili vya ujenzi wa nyumba katika vijiji vya Kororo na Nyamanzi vimeshajengwa. Aidha, Kiwanda cha Maziwa kimeshaanza kazi na mtambo wa lami umeshafungwa katika eneo la Kororo.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2016

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Mhe. Spika, mwelekeo wa ukuaji wa uchumi duniani kwa mwaka 2016 unatarajiwa kutoa matokeo tofauti kimaeneo. Kwa ujumla uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2016 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2015. Uchumi wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kubakia katika ukuaji wa kiwango cha wastani wa asilimia 1.9 kwa mwaka 2016 kama ilivyokuwa kwa mwaka 2015. Vile vile, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2015. Kukua kwa kasi

ya ukuaji wa uchumi kutatokana na uwekezaji katika makaazi, kuongezeka kwa ajira kwa nchi zilizoendelea na kuongezeka kwa shughuli za biashara kwa nchi zinazoendelea.

Mhe. Spika, uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.0 kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2015. Inakadiriwa kuwa kushuka kwa bei za bidhaa za mafuta kutaathiri ukuaji wa uchumi wa nchi wazalishaji wa mafuta katika kanda hizi zikiwemo Angola, Nigeria na Sudani ya Kusini. Vile vile, uchumi wa nchi ya Afrika ya Kusini ambayo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Afrika unatarajiwa kushuka kutokana na kupungua kwa uwekezaji kutoka nchi zilizoendelea hasa katika maeneo ya nishati na madini.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2016

Mhe. Spika, mwelekeo wa uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Mkakati Mpya wa Maendeleo wa Zanzibar 2016-2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016 uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 6.3 kutoka asilimia 6.6 mwaka 2015. Pamoja na matarajio ya kupungua kidogo kwa kasi ya ukuaji mambo yafuatayo yanatarajiwa kuchangia ukuaji huo:-

- i) Kuendelea kuimarika kwa sekta ndogo zikiwemo:-
 - Uhifadhi na usafirishaji: Hii itatokana na kuongezeka kwa shughuli katika ngazi mbali mbali za uzalishaji viwandani, biashara, ukarabati pamoja na ufugaji.
 - Sayansi, ufundi na ujuzi: Kwa kuongezeka kwa shughuli za utafiti na ubunifu.
 - Fedha na Bima: Hii itatokana zaidi na kuongezeka kwa shughuli za kifedha kwa kufunguliwa matawi ya benki mbili mpya (*Equity Bank na Bank of Africa*).
 - Habari na mawasiliano: Kwa kuongezeka kwa matumizi ya mitandao na huduma za simu.

- ii) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa mapato ya ndani yakiwemo:
 - Utekelezaji wa Sheria ya Kodi ya Majengo (*Property Tax*).
 - Udhhibiti wa Bandari bubu kuepusha biashara za magendo mbali mbali.
 - Kuyafanyia kazi mapendekezo ya kuongeza mapato yaliyoibuliwa katika Maabara ya Utafutaji Rasilimali fedha kwa ununuzi wa mashine za kutolea risiti (*EFD*).
 - Kutekeleza mikakati makhsusi kwa kila eneo la ukusanyaji.
- iii) Pia mchango mkubwa wa ukuaji wa kasi ya uchumi utatokana na kuongezeka kwa uzalishaji na usafirishaji wa karafuu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016 mambo yanayotarajiwa kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi ni pamoja na:-

- i) Kupungua kwa uzalishaji wa mazao (*crops*) katika sekta ya kilimo.
- ii) Kupungua kwa shughuli za usafirishaji wa bidhaa kutokana na kuwa mwaka 2016 ni msimu mdogo wa uzalishaji wa zao la karafuu;
- iii) Kupungua kwa kasi ya ukuzaji rasilimali nchini kutokana na matayarisho ya utekelezaji wa miradi mikubwa inayotarajiwa kuanza mwaka 2017;
- iv) Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zenye uchumi mkubwa duniani hususan nchi zilizo katika Zoni ya Ulaya ambazo zina mchango mkubwa katika soko la Utalii la Zanzibar. Miongoni mwa nchi hizo ni Italia, Ujerumani, Hispania, Ubelgiji na Ufaransa.

Mhe. Spika, kuhusiana na mfumko wa bei hali inatarajiwa kuwa tulivu na kuendelea kubakia katika tarakimu moja kutokana na sababu zifuatazo:-

- i) Kushuka kwa bei za bidhaa duniani kama vile mafuta, mchele, sukari na unga wa ngano;
- ii) Kuimarika kwa sekta ya Uvuvi kwa kuendelea kudhibiti uharibifu wa matumbawe na kuzalishwa kwa vifaranga vya

samaki; pamoja na kuendelea kupokea bidhaa ya samaki kutoka nje ambapo mwaka 2015 tumepokea jumla ya tani 495.

- iii) Serikali kuendelea kutoa punguzo maalum la ushuru kwa bidhaa muhimu za chakula;
- iv) Kuendelea kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa bei za bidhaa ili kudhibiti upandaji wa bei usio wa lazima;
- v) Kuimarika kiutulivu kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania;
- vi) Kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani na sekta ya kilimo.

MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/17

Mhe. Spika, mwaka 2016/17 ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar na vile vile kwa maendeleo ya kikanda na kidunia. Kwa upande wa Zanzibar ni mwaka ambao tunatarajia kuanza kutumia Mkakati mpya wa Maendeleo. Kwa upande mwingine kumalizika kwa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kutasaidia kutoa viashiria vilivyotumika kupima mafanikio ya utekelezaji wa MKUZA II. Serikali imekamilisha utafiti wa kujua jinsi ya kufanya mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa Zanzibar (*Zanzibar Economic and Social Transformation*), utafiti huu umependekeza mikakati minne mikubwa kwenye maeneo ya (1) Utalii (2) viwanda vidogo vidogo (3) miundombinu ya kituo cha biashara cha kuhifadhia na kufanyia shughuli za kuhifadhi na kusafirisha mizigo kama maghala na mazingira kwa ujumla.

Aidha, kidunia, mataifa yameanza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo yamechukua nafasi ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia yaliyomalizika muda wake mwaka 2015. Malengo hayo mapya yameshaingizwa katika mipango ya nchi, kupitia Mpango Mkakati Mpya wa Zanzibar ambao utanza kutumika Julai mwaka 2016.

Mhe. Spika, Mkakati Mpya wa Maendeleo wa Zanzibar 2016-2020 unakusudia kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa kuimarisha uchumi endelevu, kujenga miundombinu imara, kukuza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo, utalii na viwanda vidogo vidogo; kuimarisha rasilimali watu; ubora wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, mazingira endelevu na misingi ya utawala bora.

MAENEYO YA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2016/17

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar ni kama ifuatavyo:

Kuendeleza Miundombinu ya Msingi ya Barabara, Bandari, Viwanja vya Ndege na Nishati

Katika kuimarisha usafiri wa nchi kavu, barabara mbali mbali zitajengwa zikijumuisha kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Wete–Chake, kuendeleza ujenzi wa barabara ya Ole - Kengeja, kuanza ujenzi wa barabara ya Kwa Nyanya - Mkokotoni pamoja na kuanza ujenzi wa barabara tatu za Jendele – Cheju – Unguja Ukuu Kaebona, Kizimbani – Kiboje na Jumbi – Koani. Kwa upande wa miundombinu ya bandari, serikali inategemea kuanza ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri baada ya kukamilika kwa taratibu za masuala ya fedha na mikataba.

Aidha, serikali itaendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria (*Terminal II*) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Abeid Amani Karume wa Zanzibar kufuatia kufikia hatua za mwisho za makubaliano na wadau wa mradi huo. Uwanja wa Ndege Pemba utaendelezwa kwa kukamilisha michoro na taarifa za kina za kiufundi hatimae kuongeza urefu wa njia ya kuruka na kutua ndege utakaowezesha kutua ndege kubwa kufikia *Boeing 737* na kuimarisha vifaa na huduma muhimu za uwanja huo. Kuhusu miundombinu ya nishati, serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme katika Kisiwa cha Fundo ili kuvutia zaidi uwekezaji katika kisiwa hicho, kuendelea na Utafiti wa Nishati Mbadala wa matumizi ya upepo na nguvu za jua na kukamilisha Sheria ya Mafuta na Gesi na kuanza utekelezaji wake.

Kutekeleza Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (R4P)

Mhe. Spika, serikali itaendelea kutekeleza Programu Mjumuisho ya kuendeleza Utalii kwa kufanya utafiti wa hali ya utalii na biashara katika visiwa vya Fundo, Kokota, Njao, Bawe, *Prison Island* na Changuu; kuanza ujenzi wa vituo vya usalama na kuandaa maonyesho na matamasha ya kibiashara. Shughuli za Programu ya kuimarisha mazingira bora ya biashara zitaendelezwa kwa Ununuzi wa magazebo matano (mfano wa mashamiana matano) makubwa mawili na madogo matatu ambayo yatatumika kwa maonyesho ya kibiashara. Aidha, ununuzi wa mashine 1,000 za kutolea risiti (*Electronic Fiscal Devices - EFD*) kwa awamu ya kwanza utafanyika ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Kuimarisha Huduma za Kijamii

Mhe. Spika, ubora wa elimu ni suala muhimu katika kupata rasilimali watu yenye ujuzi na maarifa. Kwa kuzingatia hili, serikali itaanza ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya amali katika maeneo ya Daya Mtambwe na

Makunduchi; Kuanza ujenzi wa skuli 10 za ghorofa kwa ngazi ya Sekondari katika maeneo ya Chumbuni na Rahaleo (Mjini), Bububu (Magharibi A), Fuoni, Kwarara na Kinuni (Magharibi B) kwa Unguja na katika maeneo ya Wara (Chake Chake) Micheweni (Micheweni), Kizimbani (Wete) na Mwambe (Mkoani) kwa Pemba; Kuandaa maabara ya elimu itakayoibua maeneo muhimu ya utekelezaji na kupunguza changamoto za ubora wa elimu na kuanza utoaji wa huduma za chakula kwa wanafunzi katika skuli za msingi.

Mhe. Spika, kwa upande wa huduma za afya mkazo utawekwa katika ukamilishaji wa jengo la Hospitali ya Abdalla Mzee na jengo la kitengo cha huduma za watoto; kukamilisha maandalizi ya ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Mnazimmoja, kufanya matengenezo ya jengo la hospitali ya macho Mnazimmoja; kufanya matengenezo ya vituo 11 vya kutolea huduma za afya vya Daraja la Pili Unguja na Pemba na kuendelea na ujenzi wa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, upatikanaji wa maji safi na salama ni muhimu katika kulinda afya za wananchi na kuepusha maradhi mbali mbali hasa ya mripuko. Serikali itatilia mkazo uimarishaji wa miundombinu na usambazaji wa maji mijini na vijijini kwa kulaza mabomba mapya na kubadilisha mtandao wa mabomba ya zamani, kuchimba visima 10 na kuvifanyia matengenezo visima 30 Mjini Magharibi na kuanza ujenzi wa matangi 11 Unguja na Pemba. Ufungaji wa mita kubwa 33 za uzalishaji na ndogo 6,900 kwa watumiaji majumbani utafanyika.

Kuimarisha Kilimo

Mhe. Spika, kilimo cha Mazao hasa ya chakula kitaimarishwa kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya Chaani, Kinyasini, Makwararani na Mlemele. Elimu ya ufugaji itatolewa kwa vikundi vya wafugaji na kupatiwa ng'ombe na mbuzi ili kuwawezesha wafugaji wadogo wadogo kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa zinazotokana na mifugo. Kwa upande wa uvuvi, serikali itaanza ujenzi wa Soko la Malindi na kuanza matayarisho ya ujenzi wa bwawa la kufugia vifaranga vya samaki ikiwemo tathmini ya hali ya kimazingira pamoja na kuweka miundombinu ya umeme na maji kwa Kituo cha Utafiti wa Vifaranga Beit el Ras.

Kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda

Mhe. Spika, serikali ina azma ya kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya Kati (*SMEs*) ili kuongeza ajira na kuimarisha uchumi. Katika mwaka 2016/17,

Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda utatayarishwa utakaopelekea kuanzishwa kwa Programu ya Kuimarisha Viwanda nchini. Aidha, Taasisi ya Viwango Zanzibar itaimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya maabara vitavyowezesha kufanya uchunguzi wa bidhaa zinazozalishwa na kuingia nchini ili kulinda afya na usalama wa watumiaji.

Kuendeleza Programu za Kukuza Ajira kwa Vijana

Mhe. Spika, ajira kwa vijana inaendelea kutiliwa mkazo hasa katika suala la kuweza kujijari wenyewe. Katika kufikia hili, serikali inakusudia kununua boti za uvuvi na kuwapatia vijana ili waweze kuvua katika Bahari Kuu na kujipatia kipato. Aidha, elimu ya ujasiriamali itamarishwa kwa kukipatia vifaa Kituo cha Ujasiriamali Unguja na kuanza ujenzi wa Kituo kipyacha Ujasiriamali Pemba.

Kuongeza Juhudi za Kulinda Mazingira Dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kitaifa na Jamii kwa Jjumla

Mhe. Spika, suala la mazingira na mabadiliko ya tabia nchi ni muhimu hasa kwa nchi kama yetu ya visiwa. Serikali inakusudia kupanda mikoko kwa maeneo matano yaliyoathirika na kutambuliwa ya Kilimani, Tovuni, Kisiwa Panza, Ukele na Tumbe pamoja na kujenga kuta kwa maeneo mawili ya Kilimani na Kisiwa Panza.

Kufanya tafiti katika sekta mbali mbali

Mhe. Spika, tafiti ni muhimu katika kupata taarifa kwa kufanya maamuzi sahihi. Serikali inakusudia kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo utafiti juu ya kubadilisha kianzio kipyacha cha mwaka kwa Pato la Taifa na Faharisi za Bei; Utafiti juu ya Mchango wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii; Utafiti juu ya Uhusiano wa Matumizi ya Vyakula na Maradhi yasiyoambukiza na Utafiti juu ya Kuanzishwa kwa eneo la kuhifadhi aina mbali mbali za mimea ya asili inayoanza kutoweka na athari zake kwa utalii ndani na nje ya nchi.

Kuimarisha Misingi ya Utawala Bora na Kisheria

Mhe. Spika, utawala bora ni msingi muhimu katika kufikia malengo yaliyopangwa katika nyanja zote ikiwemo uwajibikaji, utii wa sheria pamoja na upatikanaji wa haki. Katika mwaka 2016/17, serikali itaandaa mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Kesi Zanzibar na kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu.

RASILIMALI NA MWELEKEO WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO 2016/17

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17, jumla ya TZS bilioni 395.9 zimepangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji programu 25 (ikiwemo programu moja mpya) na miradi 38 (miradi saba mipya) ya maendeleo. Serikali itatoa shilingi bilioni 71.1 sawa na asilimia 18 ya bajeti yote ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS bilioni 58.0 ni kwa miradi ya vipaumbele, yenye mikataba au dhima (*Commitment*) na Tzs. bilioni 13.1 kwa miradi mengine. TZS bilioni 324.8 sawa na asilimia 82 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa shilingi bilioni 93.3 ni ruzuku na TZS bilioni 231.5 ni mkopo. Programu na miradi hiyo imejikita kupata matokeo katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo:-

Kuwezesha Ukuaji wa Uchumi Jumuishi na Endelevu kwa Sekta Kubwa zote

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha mazingira bora yatakayosaidia ukuaji wa uchumi endelevu ili kupambana na umasikini uliokithiri na kupunguza umasikini wa kipato. Matarajio ya muda wa kati wa eneo hili ni kuwa na mazingira rafiki kwa ukuaji wa sekta binafsi na upatikanji wa ajira, kuwa na uwekezaji wa umma unaotosheleza ili kusaidia miundombinu ikiwemo ya mawasiliano na vichocheo vyengine vya uchumi, kuwa na sekta yenye ushindani ya utalii yenye manufaa endelevu na jumuishi kwa Wazanzibar, kuwepo na uzalishaji wa kisasa katika sekta za kilimo na viwanda kwa kuongeza thamani (*value addition*) na kuwepo sekta binafsi iliyoshamiri.

Mhe. Spika, eneo hili limepangiwa kutekeleza jumla ya programu 13 na miradi 12 (programu moja ni mpya) ambapo limetengewa jumla ya TZS 225.38 bilioni sawa na asilimia 57 ya Bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, serikali imetenga TZS bilioni 31.04 na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 194.34 bilioni.

Kukuza Uwezo wa Watu

Mhe. Spika, mkakati mpya unakusudia kuimarisha uwezo wa watu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Eneo hili lina matarajio ya kuongeza ajira kwa watu wote (vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na kadhalika) mijini na vijijini kwa kuendeleza maarifa yao na kuongezeka uwezo wa wajasirimali ili kuimarisha fursa za kuweza kujijiri.

Mhe. Spika, eneo hili limepangiwa kutekeleza jumla ya programu mbili na mradi mmoja ambapo limetengewa jumla ya TZS bilioni 1.05 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, serikali imetenga TZS milioni 600.0 na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS milioni 450.0.

Kutoa Huduma Bora Kwa Wote

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za kisasa kwa jamii. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na huduma bora za afya na usafi wa mazingira, maji safi na salama, na kupambana na maradhi yenye kuambikiza na yasiyoambukiza; kuwa na elimu bora kwa wote na jinsia zote; kuwa na makaazi bora, matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa nishati; kuwa na uhibitaji wa unyanyasaji wa watoto na wanawake; kuwa na uwezo na utayari wa kupambana na majanga/dharura za aina zote; kuwa na usalama wa upatikanaji wa chakula kwa jamii yote.

Mhe. Spika, eneo hili limepangiwa kutekeleza jumla ya programu saba na miradi 18 (miradi mipya mitatu) ambapo limetengewa jumla ya shilingi bilioni 129.53 sawa na asilimia 33 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, serikali imetenga TZS bilioni 13.07 na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS bilioni 116.46.

Kuwepo Mazingira Endelevu na Uhimili wa Mabadiliko ya Tabia Nchi

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha uwezo wetu wa kukabiliana na mabadiliko ya mazingira na tabia nchi. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na uwezo wa kutosha wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi; kuwa na uhifadhi wa viumbe vya baharini na nchi kavu na kupunguza upotevu wake; kuzuia uharibifu wa mazingira na kupunguza athari za kijamii zinazotokana na shughuli za kiuchumi.

Mhe. Spika, eneo hili limepangiwa kutekeleza jumla ya miradi mitano mipya ambapo limetengewa jumla ya TZS bilioni 3.99 sawa na asilimia 1.0 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, serikali imetenga TZS 100.0 milioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 3.89 bilioni.

Kushikamana na Misingi ya Utawala Bora

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha misingi ya utawala bora, haki na sheria katika ngazi zote. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na mifumo ya kiutawala na kitaasisi yenye kuwajibika, iliyowazi na ambayo inaendeshwa bila ya rushwa; kufikia usawa na uwiano wa kijinsia, jamii jumuishi na uwezeshaji

wa wanawake, watoto wa kike, vijana, watu wenye ulemavu na watu walio katika mazingira hatarishi; kuwa na upatikanaji wa haki, kuheshimu utawala wa sheria, haki za msingi za binadamu na ushirikishwaji katika mchakato wa demokrasia; kuwa na uwajibikaji wa mashirika kwa jamii na kuwa na mazingatio zaidi ya watu katika mipango.

Mhe. Spika, eneo hili limepangiwa kutekeleza jumla ya programu nne na miradi 10 ambapo limetengewa jumla ya TZS 35.95 bilioni sawa na asilimia 9 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, serikali imetenga Shilingi 26.24 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 9.71 bilioni.

Ufuatiliaji na Tathmini kwa Programu na Miradi ya Maendeleo

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17, masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo yatatiliwa mkazo na kusimamiwa ipasavyo na serikali. Katika kufikia malengo yaliyokusudiwa, serikali itaandaa Muundo wa Ufuatiliaji na tathmini wa Mkakati Mpya na kusimamia utekelezaji wake kitaifa. Aidha, itaandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya maendeleo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, hitimisho la hotuba yangu hii haliwezi kukamilika bila ya shukurani za kipekee kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Ndugu Juma Hassan Reli, Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini, Kamishna wa Ukuzaji Uchumi, Kamishna wa Ufuatiliaji na Tathmini na Kamishna wa Mipango na Maendeleo ya Watendakazi kwa kusimamia kwa umahiri kazi za kila siku za Tume ya Mipango na maandalizi ya hotuba hii. Pia, natoa shukurani kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Watendaji wake wote kwa kutupatia takwimu kwa ajili ya matayarisho ya hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba pia kumshukuru kwa dhati kabisa Katibu Mkuu, Ndugu Khamis Mussa Omar na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kufanya kazi kubwa kwa mashirikiano makubwa na Tume ya Mipango. Aidha, natoa shukurani kwa Makatibu Wakuu wa wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watendaji wao wote kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika mchakato mzima wa utayarishaji wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo. Ni matumaini yangu kwamba tutashirikiana zaidi katika utekelezaji wa kazi katika siku zijazo.

Mhe. Spika, kwa aina ya kipekee naomba kuyashukuru Mashirika ya Kitaifa, Kimataifa na Nchi Wahisani kwa misaada ya kifedha na kiutaalamu wanaoendelea kutupatia wakiwemo *AfDB, ACRA, BADEA, CARE AUSTRIA, CDC, CHAI, CHINA, CANADA, CIDA, COSTECH, DFID, EAC, EGH, EGYPT, EU, EXIM BANK, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GERMANY, GLOBAL FUND, GRFC, GPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, OPEC, ITC, JAPAN, JICA, KOREA, MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, PMI, RAS - AL - KHAIMAH, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SWEDEN, UK, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, UNIDO, URT, USA, USAID, UN-HABITAT, UN WOMEN, WB, WHO* na *WIPO*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mapendekezo ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono takriban na Baraza zima. Sasa shughuli inayofuata Waheshimiwa Wajumbe ni shughuli ya bajeti, lakini sasa, kabla sijasitisha hizi shughuli naomba nimuombe Mwanasheria Mkuu au Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili atupe neno kidogo. Mheshimiwa, tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kabla ya kusema nililokusudia nilitamke mbele ya Baraza lako, naomba pia kukupa taarifa kutokana na kifo kilichotokea cha Balozi Mdogo wa Oman aliyepo Zanzibar na ambaye anatarajiwa mwili wake kusafirishwa kupelekwa Oman mchana huu leo saa tisa. Kwa hivyo, kwa hudhuni kubwa kwa niaba ya serikali na Baraza lako tukufu tunatoa salamu zetu za pole kwa Serikali ya Watu wa Oman, Mfalme wa Oman na jamaa na familia yote ya marehemu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa uniruhusu tuweke kando Kanuni ya 23(4) ili tuweze kuakhirisha shughuli zetu za Baraza asubuhi hii na tuweze kuendelea leo jioni saa kumi kwa ajili ya hotuba ya bajeti.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na sasa naomba nichukue nafasi hii niwahoji ili tuweke kando kanuni ya muda na kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kusitishwa mapema, lakini pia kuturuhusu ili tuweze kurudi tena saa kumi jioni kwa ajili ya kuja kusikiliza Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Waheshimiwa, naomba niwahoji wale wote wanaounga mkono hoja hii wanyanyue mikono yao. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5.26 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 10:00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango lakini ninawaomba sasa wapambe wa Spika ili waweze kumsindikiza Mhe. Waziri ili aje awasilishe hoja yake ya bajeti.

*(Hapa Wapambe wa Spika walikwenda kumchukua
Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na kuingia naye ukumbini)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango karibu sana.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati Maalum ya kujadili mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, niruhusu nianze, kama ilivyo ada yetu waumini, kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu wetu muumba, kwa neema zake zote anazoendelea kuturuzuku, ikiwemo ya uhai, afya njema, amani na utulivu. Ni kwa neema hizi ambazo nyingi hatuna uwezo nazo, ndio leo hii tumeweza kukutana hap.

Kukutana huku kutatuwezesha kutimiza matakwa ya Katiba yetu inayotutaka kujadili mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha, yakiwasilishwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kuanza kutoa pongezi na shukrani. Kwanza, nianzie kwa kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wetu wa Zanzibar ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nampongeza Dkt. Shein kwa kuchaguliwa tena na wananchi walio wengi kuiongoza tena nchi yetu kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Sote tunafahamu kuwa kuchaguliwa huku kunatokana na imani kubwa waliyonayo wananchi kwake, kutokana na kazi kubwa aliyofanya katika awamu ya kwanza ya uongozi wake. Namuomba kipindi chengine cha utendaji uliotukuka, wenye uadilifu, hekma na mafanikio makubwa zaidi. Mwenyezi Mungu amuongoze kututumikia vyema wananchi sote, AMIN.(Makofi).

Mhe. Spika, niruhusu pia nimpongeze sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais, mosi, kwa kuendelea kuaminiwa mara hii na wananchi wa Jimbo jipya la Mahonda. Kwa kumuamini na kumkubali kwao wamemchagua kuwa Mwakilishi wao katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu. Pili, nampongeza kwa kuendelea kupata imani ya Mhe. Rais ambaye amemteua tena kuwa Makamu wake wa Pili wa Rais. Namtakia utendaji thabiti, wa mafanikio na mfano kwetu sote.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie fursa hii kukupongeza sana wewe binafsi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo ya kuliongoza Baraza letu hili la Tisa. Nawe pia umepata imani ya Wajumbe wa Baraza hili, na ni imani yangu kuwa katika kipindi chako tutashuhudia utendaji wa hali ya juu wa Baraza hili na kuimarika zaidi mahusiano yake na mihimili mengine ya dola. (Makofi).

Mhe. Spika, pongezi zangu za dhiti zinakwenda pia kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili, waliochaguliwa na wananchi, walioteuliwa kupitia viti maalum na walioteuliwa na Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa matakwa ya Katiba yetu. Nawapongeza pia Waheshimiwa wote waliopata fursa ya kuteuliwa na Mhe. Rais kuziongoza Wizara mbali mbali. Nao wote nawatakia utendaji bora zaidi katika kuwahudumia wananchi wote.(Makofi).

Mhe. Spika, pongezi zote hizi zinafuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa marudio wa Machi 20 mwaka huu 2016, kutokana na matatizo yaliyojitokeza

na kufutwa uchaguzi wa awali na Tume ya Uchaguzi. Uchaguzi Mkuu ulifanyika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuiongoza Jamhuri yetu ya Muungano kama Rais wake wa Tano tokea kuasisiwa kwa Muungano. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tayari Mhe. Magufuli amejipambanua kwa uchapaji kazi wake na kutovumilia uzembe, ubadhirifu na wizi wa mali za umma. Kwa hakika kauli mbiu yake ya “Hapa Kazi Tu” tayari imedhihirika kitendo katika kipindi kifupi cha uongozi wake wa nchi yetu. Tunamuomba uongozi mwema na wa mafanikio, yeye na wasaidizi wake wakuu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa upande wa shukrani, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kunituua kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ndio roho na moyo wa maendeleo ya nchi yetu.

Shukrani pia ziende kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa utulivu wao mkubwa wanaouonesha na ukomavu wao kwa nyakati zote, hata pale penye majaribu ya kijamii na kisiasa kama ilivyojitokeza mara hii katika Uchaguzi wetu Mkuu. Bila ya shaka yoyote, napenda kuvishukuru vyama vyote vya siasa na viongozi wake, hususan Chama Cha Mapinduzi, kwa ustahamilivu mkubwa wa kisiasa na kuivusha salama Zanzibar katika kipindi hicho. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Zanzibar imeandika historia mpya ya siasa, Zanzibar imeandika zama mpya za utulivu, Zanzibar imeandika ukurasa mpya wa demokrasia. Naamini kuwa, kwa yeyote mwenye kutafakari kwa makini na bila ya kuegemea upande wowote, atabaini mafunzo mengi ya kisiasa, kidemokrasia na kijamii katika mambo ambayo tumepitia katika kipindi hicho mpaka kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Marudio wa tarehe 20 Machi 2016 na hata baada ya hapo.

Mhe. Spika, niruhusu pia nitoe shukrani za aina ya pekee kwa wananchi wote wa Jimbo la Donge, kwa kunichagua kwa kauli moja kuwawakilisha katika Baraza lako hili tukufu la kutunga Sheria. Nimeupokea kwa unyenyekevu mkubwa uteuzi wa Mhe. Rais na wa wananchi wa Donge. Najua dhima niliyonayo na ninamuomba *Allah* kuniwezesha kwa kila hali kuwatumikia vyema wananchi wote wa Zanzibar kwa dhamana niliyopewa ya Uwaziri wa Fedha na Mipango, na ule wa Jimbo langu la Donge kwa dhamana ya kuwawakilisha katika Baraza hili. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nianze kwa kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16.

HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO

Mhe. Spika, asubuhi ya leo nilieleza mwenendo wa uchumi wetu kwa mwaka uliopita wakati nikiwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015. Sikusudii kurejea maelezo niliyoyotoa awali. Naomba tu niseme kuwa kwa mwaka 2015, pato letu la nchi limefikia TZS 2,308.0 bilioni kwa bei za mwaka huo sawa na TZS 1,169.0 bilioni kwa bei za kudumu za mwaka 2007. Kwa miaka mitano iliyopita, uchumi wetu umekuwa kwa wastani wa asilimia 7.0. Kwa bei za kudumu za mwaka 2007, wastani wa pato la mtu binafsi nao umefikia Dola 674 za Marekani, sawa na Dola 817 kwa bei za mwaka 2015. Wakati tukijipanga kuendeleza mageuzi ya kiuchumi, tunapaswa kujua kuwa tunaanzia na kiwango hicho cha uchumi wetu.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Ofisi yake ya Mtakwimu Mkuu imekamilisha Utafiti wa Kipato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2015. Kazi hii imehusisha pia wataalamu kutoka nje na ilianza na mapitio ya njia inayotumika kupima umaskini kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya Zanzibar. Matokeo ya awali yanaonesha mafanikio katika jitihada zetu za kupunguza umaskini, zikionesha kuwa wananchi wanaoishi chini ya kiwango cha mahitaji wamepungua kutoka asilimia 34.9 mwaka 2010 hadi asilimia 30.4 mwaka 2015. Aidha, watu wanaoishi kwa umaskini wa chakula wamepungua nao kutoka asilimia 11.7 hadi asilimia 10.8. Kiwilaya, bado jitihada zinahitajika zaidi kwa Wilaya ya Micheweni Pemba, kwani imeendelea kuongoza ikifuatiwa na Wilaya nyengine za Pemba. Kiwango cha chini zaidi cha umaskini kwa sasa kimejitokeza katika Wilaya ya Magharibi. Matokeo haya ya utafiti yanahitaji juhudi maalum katika miaka mitano ijayo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16

Mapitio ya Mapato

Mhe. Spika, kwa mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya TZS 830.4 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 450.5 bilioni ni mapato ya ndani na TZS 349.9 bilioni kutokana na ruzuku na mikopo kutoka nje. Ili kuziba nakisi ya bajeti, Serikali iliidhinisha kukopa ndani TZS 30.0 bilioni.

Mhe. Spika, makusanyo halisi kwa kipindi cha miezi tisa hadi Machi 2016, yamefikia TZS 399.0 bilioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, kati ya mapato hayo, jumla ya TZS 306.1 bilioni zimekusanywa kutokana na vyanzo vya ndani sawa na asilimia 68 ya lengo la miezi tisa. Ukusanyaji huu unamaanisha ongezeko la mapato ya ndani kwa TZS 31.1 bilioni ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 275.0 bilioni yaliyopatikana katika kipindi kama hicho hadi Machi 2015, sawa na ukuaji wa asilimia 11.3.

Mhe. Spika, pamoja na ongezeko hilo la mapato, lengo la ukusanyaji kwa kipindi hicho halikufikiwa. Sababu kuu za kutofikia lengo la ukusanyaji ni pamoja na hizi zifuatazo:

- i. Kuchelewa kwa marejesho ya Kodi ya VAT kutoka SMT kwa sababu ya Sheria mpya ya VAT ya Tanzania Bara iliyofuta kipengele cha marejesho ya fedha hizo;
- ii. Kupungua kwa uingizaji wa bidhaa nchini, hususan magari; na
- iii. Kupungua kwa idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar kwa asilimia 5.7.

Mapato ya Kodi

Mhe. Spika, kati ya mapato ya ndani, mapato kutokana na kodi yamefikia TZS 288.5 bilioni, sawa na asilimia 88.8 ya lengo la TZS 324.9 bilioni. Ukusanyaji huo pia unaashiria ukuaji wa mapato kwa asilimia 11 sawa na TZS 46.0 bilioni kutoka TZS 242.5 bilioni zilizokusanywa hadi Machi mwaka 2015.

Utendaji wa *ZRB* umefikia asilimia 85.4 ya lengo baada ya kukusanya TZS 141.3 bilioni wakati lengo lilikuwa ni TZS 165.4 bilioni. Athari niliyoeleza awali ya kutorejeshwa fedha za VAT kwa bidhaa zitokazo Tanzania Bara imejitokeza katika kiwango cha utendaji wa *ZRB*. Hali hii pia imepelekea ukuaji mdogo wa mapato wa asilimia 4.1 kutoka TZS 135.7 bilioni za mwaka jana.

Mhe. Spika, kwa upande wa *TRA*, makusanyo halisi ya kodi kwa miezi tisa hadi Machi 2016 yamefikia TZS 121.0 bilioni, sawa na asilimia 91.4 ya lengo la kukusanya TZS 132.4 bilioni. Hata hivyo, ikilinganishwa na utendaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2014/15, kunajitokeza ongezeko la asilimia 13.7 sawa na TZS 14.2 bilioni kutoka TZS 106.8 bilioni za mwaka jana. Kati ya makusanyo hayo, Idara ya Forodha imemudu kukusanya TZS 72.4 bilioni kati ya lengo la TZS 85.1 bilioni kwa kipindi hicho, sawa na utendaji wa asilimia 85.1. Idara ya Kodi za Ndani imeweza kuvuka lengo kwa kukusanya TZS 48.6 bilioni wakati lengo ni TZS 47.3 bilioni.

Mapato yasiyo ya Kodi

Mhe. Spika, kati ya mapato ya ndani, Serikali ilitarajia kukusanya TZS 25.0 bilioni kutokana na mapato yasiyo ya kodi. Makusanyo halisi kutokana na Wizara mbali mbali za Serikali kwa kipindi cha miezi tisa yamefikia TZS 17.6 bilioni, sawa na asilimia 103 ya lengo la kukusanya kipindi hicho la TZS 17.0 bilioni. Ukusanyaji huo unamaanisha ukuaji wa mapato kutoka chanzo hicho kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka jana kipindi kama hicho ya TZS 16.7 bilioni.

Mikopo ya Ndani

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa, Julai hadi Machi 31 mwaka huu, Serikali imekopa ndani jumla ya TZS 10.0 bilioni, ikiwa ni asilimia 33 ya fursa ya kukopa TZS 30 bilioni iliyo dhinishwa. Kiasi hicho kinashabihiana na mikopo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa 2014/15.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, mapato kutoka nje yalifikia TZS 82.8 bilioni. Jumla ya TZS 75.1 bilioni ni ruzuku na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 22 tu ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, Ruzuku ni TZS 37.9 bilioni na Mikopo ni TZS 37.2 bilioni. Kiasi kilichobakia cha TZS 7.7 bilioni ni Misaada ya Kibajeti (*GBS*).

Mhe. Spika, kama inavyojitokeza, kwa ujumla, ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha mapitio umeathiriwa zaidi na mwenendo usioridhisha wa mapato ya nje uliosababishwa zaidi na kuendelea kusuasua kwa utekelezaji wa miradi mikubwa kama vile ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar, ujenzi wa barabara za Kati Unguja, na mradi wa kuimarisha usalama ikiwemo uwekaji wa Kamera za *CCTV*.

Mapitio ya Matumizi

Mhe. Spika, mwenendo wa mapato umeathiri utekelezaji wa bajeti kimatumizi. Hadi Machi 31 mwaka 2016, matumizi halisi yalifikia TZS 352.9 bilioni, yakijumuisha TZS 298.4 bilioni za matumizi yatokanayo na mapato ya ndani na TZS 54.5 bilioni matumizi yatokanayo na mapato ya nje. Matumizi kwa ajili ya kazi za kawaida yalifikia TZS 283.8 bilioni, sawa na asilimia 66 ya lengo la mwaka kama ifuatavyo:

- i. Mishahara TZS 145.6 bilioni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka;
- ii. Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 66.5 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya mwaka;
- iii. Ruzuku kwa Taasisi mbali mbali TZS 36.0 bilioni sawa na asilimia 63; na
- iv. Matumizi mengineyo TZS 35.6 bilioni sawa na asilimia 42 ya makisio ya mwaka.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho cha mapitio, matumizi ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 69.1 bilioni, sawa na asilimia 17 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, fedha kutokana na Washirika wa Maendeleo ni TZS 54.5 bilioni, sawa na asilimia 16 ya makadirio ya mwaka wakati mchango wa serikali umefikia TZS 14.60 bilioni sawa na asilimia 28 ya makadirio.

Matarajio ya Mapato Julai – Juni 2015/2016.

Mhe. Spika, haitarajiwi kuwa Miradi mikubwa iliyopata changamoto wakati wa utekelezaji itapata ufumbuzi katika kipindi kilichobakia cha Bajeti. Kwa sababu hiyo, na kwa kuzingatia mwenendo wa mapato ya ndani, matarajio ya makusanyo ya mapato hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni 2016 ni kukusanya TZS 516.0 bilioni, sawa na asilimia 62 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 830.4 bilioni.

Mhe. Spika, mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 412.5 bilioni, sawa na asilimia 91.6 ya makisio ya TZS 450.5 bilioni. Kati ya kiasi hicho, *TRA* inatarajiwa kukusanya TZS 163.7 bilioni, sawa na asilimia 91.7 ya makadirio ya mwaka. Mapato kutoka *ZRB* yanatarajiwa kufikia TZS 204.3 bilioni sawa na asilimia 90.4 na makusanyo ya Mawizara ni TZS 23.4 bilioni, sawa na asilimia 119.5. Kodi ya Mapato (*PAYE*) kutoka *SMT* inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na lengo.

Mhe. Spika, kutokana na sababu zilizoelezwa awali, mikopo na ruzuku kutoka nje inatarajiwa kufikia jumla ya TZS 84.3 bilioni sawa na asilimia 24 tu ya makadirio ya mwaka.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16, serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani. Utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

Kodi ya Miundombinu (*Infrastructure Tax*)

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi liliidhinisha uanzishwaji wa kodi ya Miundombinu (*Infrastructure Tax*) kwa lengo la kuimarisha miundombinu nchini. Ada zifuatazo zimetokelezwa kama zilivyoidhinishwa:

- i. Dola moja ya Kimarekani kwa siku kwa kila mgeni atakayelala katika hoteli za Zanzibar.
- ii. TZS 2,000 kwa kila abiria anayeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda katika Bandari nyengine za Tanzania nje ya Zanzibar, na TZS 1,000 kwa kila abiria anayeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda katika Bandari nyengine za Zanzibar. TZS 2,000 kwa kila abiria anayeondoka katika kiwanja cha ndege kilichopo Zanzibar na kwenda kiwanja chengine ndani ya Tanzania.
- iii. Asilimia 3 ya thamani za bidhaa zinazoingizwa nchini.
- iv. Asilimia 2 katika mauzo ya umeme.
- v. TZS 100/= ya ziada kwa lita ya petroli au dizeli inayoingizwa nchini.

Mhe. Spika, kwa ujumla, Bodi ya Mapato Zanzibar imefanikiwa kukusanya TZS10.5 bilioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya miezi tisa ya lengo la TZS 11.4 bilioni hadi kufikia Machi 2016. TRA kwa upande wake imekusanya jumla ya TZS 5.96 bilioni sawa na asilimia 79.5 ya lengo la TZS 7.5 bilioni kwa kipindi cha miezi tisa.

Ada ya viwanja vya ndege na Bandari (Sheria ya Ada ya Bandari Namba 2 ya Mwaka 1999)

Mhe. Spika, serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ili kuongeza rasmi ada hiyo kutoka dola 8 za Kimarekani hadi kufikia dola 9 za Kimarekani, ambayo tayari ilikuwa inatozwa na Kampuni za Ndege kwa kutumia Sheria ya Tanzania Bara. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS 4.47 bilioni

zimekusanywa katika kianzio hicho ambacho ni sawa na ukuaji wa asilimia 45.6 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 3.1 bilioni kwa mwaka uliopita katika kipindi kama hicho.

Mhe. Spika, Aidha, serikali imeongeza tozo la mauzo ya tiketi na usafirishaji wa mizigo baharini kutoka asilimia 5 ya kabla hadi asilimia 8 kama ilivyoidhinishwa. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS 1.84 bilioni zimekusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 94.4 ya lengo la mwaka la TZS 1.95 bilioni.

Kufanya Mapitio ya Viwango vya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Taasisi za Serikali

Mhe. Spika, serikali ilifanya mabadiliko ya viwango vya ada na tozo mbali mbali katika taasisi zake, kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi na kuvifanya viwango hivyo viendane na wakati. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 900 milioni zimekusanywa kutokana na mabadiliko ya viwango hivyo ikilinganishwa na lengo la TZS 600 milioni kwa miezi 9, sawa na asilimia 150 ya lengo.

Sheria ya Biashara (Ada ya Uingizaji wa Magari)

Mhe. Spika, serikali ilikubali kuweka kiwango mbadala cha ama TZS 100,000 kwa gari au asilimia 3 ya thamani ya gari inayoingizwa kwa kufuata kiwango kinachotoa mapato zaidi. Jumla ya TZS 710 milioni zimekusanywa katika kipindi cha mapitio, sawa na asilimia 60.6 ya makadirio ya mwaka.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, kutokana na mikopo mipya, malimbikizo ya deni la kiinua mgongo, wazabuni na kudhoofika kwa shilingi ya Tanzania kwa kulinganisha na dola ya Kimarekani, deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 25.7 hadi TZS 398.6 bilioni mwisho wa mwezi wa Machi 2016 kutoka TZS 317.2 bilioni za Machi 2015. Deni la nje limekuwa kwa asilimia 26 kutoka TZS 211.8 bilioni hadi TZS 266.8 bilioni katika kipindi hicho. Aidha, deni la ndani nalo limekuwa kwa asilimia 31.1 kutoka TZS 99.3 bilioni hadi TZS 130.2 bilioni, likiathiriwa zaidi na malimbikizo ya deni la Kiinua mgongo na lile la Hati Fungani.

Mhe. Spika, pamoja na kuongezeka huko kwa deni letu, bado kiwango hicho ni endelevu na kinachoashiria kuwa serikali ina uwezo wa kulilipa. Kwa kulinganisha na pato la taifa, deni hilo ghafi ni uwiano wa asilimia 17.3 tu ya pato la taifa la mwaka 2015.

MUSTAKABALI WA UCHUMI NA MAPATO

Mwelekeo wa Uchumi

Mhe. Spika, dira ya maendeleo ya kiuchumi imeelezwa vyema katika hotuba ya uzinduzi wa Baraza hili la Tisa iliyotolewa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kimsingi, bado dira yetu ni kufikia uchumi wa kipato cha kati. Mhe. Rais pia ameeleza haja ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ili isipungue asilimia 8 kwa mwaka. Jitihada zetu zitaelekezwa katika kushajiisha uwekezaji, uimarishaji wa sekta za uchumi kama vile huduma, hususan utalii, mageuzi ya viwanda na kilimo, ikiwemo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

Mhe. Spika, mageuzi haya ya kiuchumi yataletwa kupitia utekelezaji wa Mkakati mpya wa maendeleo uliochukua nafasi ya MKUZA II. Kama nilivyoeleza wakati wa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo, moja ya eneo muhimu la matokeo katika mkakati huo mpya ni la mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi haya yanakusudia kuimarisha sekta zote hizo nilizozitaja kwa kuzingatia uhusiano wa sekta hizo katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

Mustakabali wa Mapato

Mhe. Spika, mustakabali wa mapato ya serikali kwa miaka mitano ijayo umejikita zaidi katika kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mwelekeo huu unaendana na dhamira ya serikali ya kuongeza kujitegemea na kupunguza kadiri iwezekanavyo utegemezi wa Washirika wa Maendeleo katika kuhudumia Bajeti ya Serikali. Ni muhimu kuelewa kuwa hatufungi milango ya mashirikiano na Washirika wa Maendeleo. Mashirikiano na wao hayatasitishwa, na pale watakapotusaidia tutaendelea kupokea misaada. Hata hivyo, lengo kuu ni kujitegemea wenyewe. Katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza hili, Mhe. Rais alieleza kuwa lengo la serikali ni kukusanya TZS 800 bilioni ifikapo mwaka 2020/21 kutokana na mapato ya ndani kutoka TZS 362.8 bilioni zilizokusanywa mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, jitihada zinazochukuliwa kwa sasa ni kuhakikisha kuwa lengo hilo lililotamkwa na Mhe. Rais sio tu kuwa linafikiwa bali linafikiwa mapema zaidi katika kipindi hicho, kabla ya mwaka 2020/21. Sisi tunaamini kuwa hili linawezekana. Wenye dhamana ya kulisimamia hili tunaahidi kutimiza wajibu wetu ili liwezekane.

MWELEKEO WA BAJETI, 2016/17

Mhe. Spika, bado nchi yetu ni maskini na wananchi wanaitegemea serikali yao kuwaletea maendeleo na kuwatoa katika umaskini. Hali hii inahitaji kuendelea kuwekeza katika huduma muhimu za jamii na mageuzi ya kiuchumi. Ili kukidhi mahitaji haya ya jamii, lengo kuu la Bajeti ya Serikali litaendelea kuwa ni kujenga jamii iliyoelimika, yenye siha na yenye uhakika wa chakula, uwezo wa kiuchumi na inayothamini na kufuata misingi ya utawala bora.

Mhe. Spika, matumizi ya serikali yataendelea kuelekezwa katika kuimarisha na kuendeleza maeneo yaliyozingatiwa katika Bajeti iliyopita yakiwemo:

- (i) Huduma za Elimu
- (ii) Huduma za Afya na ustawi wa jamii
- (iii) Miundombinu ya msingi; na
- (iv) Utawala bora.

Mhe. Spika, mustakabali huo wa Bajeti umejiegemeza katika utekelezaji wa mambo yafuatayo:

- i. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015;
- ii. Mkakati mpya wa Maendeleo unaochukua nafasi ya MKUZA II unaozingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu, (*Sustainable Development Goals – SDGs*) na Mpango wa Mageuzi ya Kiuchumi;
- iii. Dira na uono wa Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kama ilivyoelezwa katika Hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza hili la Tisa la Wawakilishi tarehe 5 Aprili 2016;

Mwelekeo wa Mapato

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, jumla ya TZS 482.4 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka 2016/17 kutoka katika vianzio vya ndani kwa mchanganuo ufuatao:

- i. ZRB: inatarajiwa kukusanya TZS 237.4 bilioni
- ii. TRA: inatarajiwa kukusanya TZS 188.8 bilioni
- iii. Mapato ya mawizara: TZS 26.4 bilioni
- iv. Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT: TZS 21.0 bilioni
- v. Gawio la faida kutoka BOT: TZS 4.0 bilioni
- vi. Mgao wa faida kutoka kwenye Mashirika ya Serikali: TZS 4.8 bilioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17, serikali inatarajia kupokea ruzuku ya TZS 93.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kukopa nje jumla ya TZS 231.5 bilioni na hivyo kufanya mapato kutoka nje kufikia TZS 324.8 bilioni. Aidha, serikali inatarajia kupokea TZS 1.3 bilioni zikiwa ni fedha kutokana na misamaha ya madeni (MDRI).

Mhe. Spika, pamoja na fedha hizo zinazotarajiwa kupatikana kwa ajili ya kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo, miradi ifuatayo imefikia hatua za mwisho za maandalizi na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha baada ya kuidhinishwa rasmi. Kwa sasa Miradi hiyo inaoneshwa katika Bajeti kwa utaratibu wa 100T ili kuepusha haja ya Bajeti ya ziada *Supplimentary Budget*. Miradi hiyo ni hii ifuatayo:

- i. Mradi wa kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji unaofadhiliwa na Benki ya *Exim* ya Korea;
- ii. Mradi wa barabara za kuingia mjini unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*);
- iii. Mradi wa Ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri chini ya ufadhili wa Benki ya *Exim* ya China;
- iv. Mradi wa *e-government* awamu ya pili.
- v. Mradi wa Kuimarisha Elimu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia;
- vi. Mradi wa Huduma za Mijini awamu ya pili chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia; na

vii. Mradi wa Kuimarisha Nishati na Mafuta na Gesi Asilia unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, upatikanaji wa fedha za misaada ya kibajeti (*GBS*) bado hauna uhakika. Hivyo, kama ilivyokuwa kwa mwaka unaomalizika wa fedha, chanzo hiki kitaendelea kutoingizwa moja kwa moja katika mapendekezo ya mapato na badala yake nacho kuingizwa kwa utaratibu wa 100T.

Mhe. Spika, kwa muhtasari, kutokana na maelezo ya hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2016/17 serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 841.5 bilioni zikiwemo TZS 482.4 bilioni zitokanazo na vianzio vya ndani, mikopo ya ndani ni TZS 33.0 bilioni, TZS 324.8 bilioni za kutoka nje, na TZS 1.3 bilioni misamaha ya madeni.

Mwelekeo wa Matumizi

Mhe. Spika, kutokana na mwelekeo wa hali ya fedha (*fiscal capacity*), sera kuu ya matumizi inahitaji kubana zaidi matumizi kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo. Kutokana na mwelekeo huo, mkazo katika matumizi utalenga katika mambo yafuatayo:

- i. Kumaliza/kupunguza madeni hasa ya kiinua mgongo, walimu, wazabuni na Dhamana za Hazina;
- ii. Kuendeleza jitihada za uimarishaji wa huduma za jamii hasa elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama;
- iii. Kutekeleza miradi mikubwa na yenye tija kama vile ukamilishaji wa jengo jipya la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa A.A. Karume na barabara ya Chake – Wete na nyenginezo; na
- iv. Utekelezaji wa Mpango wa mageuzi ya Kiuchumi.

Mhe. Spika, serikali pia itaendelea na jitihada zake za kuwaenzi wazee kwa kuendelea kutoa pencheni maalum (*universal pension*) kwa wazee waliofikia umri wa miaka sabini na zaidi. Napenda kulitangazia Baraza lako tukufu kuwa serikali imeshaanza kuwalipa wazee hao Unguja na Pemba, pencheni ya shilingi 20,000/= kwa kila mwezi kuanzia mwezi Aprili mwaka huu (2016). Jitihada hizi ni endelevu katika kutunza hali na kuimarisha maslahi ya wazee wetu.

Mhe. Spika, pamoja na dhamira ya kubana matumizi, serikali pia imekusudia kutekeleza ahadi yake ya kuimarisha maslahi ya wafanyakazi wake, hususan wa kipato cha chini, ili waweze kumudu vyema maisha na kuhamasika

kufanya kazi kwa bidii zaidi. Bajeti inayopendekezwa inakusudia kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ya kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 150,000. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kurejea hapa. Bajeti inayopendekezwa inakusudia kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ya kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 150,000 cha sasa hadi TZS 300,000 katika mwaka wake wa kwanza wa kipindi hiki cha pili cha uongozi wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nitamke rasmi kuwa marekebisho hayo ya mshahara yatafanyika kuanzia mwezi Aprili 2017. Kama ilivyoahidiwa, nyongeza hii itanufaisha zaidi wafanyakazi wa kada za chini ambao ndio walio wengi. Hatua hii itasaidia pia kuimarisha maslahi ya wafanyakazi hao wakati wanapomaliza utumishi wao kwa kustaafu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, serikali pia imesikia kilio cha wafanyakazi cha kupunguziwa kodi katika kipato cha mshahara na kuwekwa sawa viwango vyake na Tanzania Bara. Hivyo, sambamba na hatua ya kupandisha kima cha chini cha mshahara, kuanzia mwezi huo wa Aprili 2017, serikali pia itafanya marekebisho ya kodi ya mapato kwa kupunguza kiwango wanachotozwa watu wa kipato cha chini kutoka asilimia 13 ya sasa hadi kufikia asilimia 9. Lengo la hatua hii ni kuimarisha kipato cha mfanyakazi wa kima cha chini kwa kumbakishia kipato zaidi ili kukidhi mahitaji ya maisha.

Mhe. Spika, Serikali inachukua hatua hizi ikielewa mzigo mkubwa inaobeba wa kibajeti. Athari ya hatua hii sio tu kuongeza sana Bajeti ya mishahara na hivyo kupunguza uwezo wake katika matumizi mengineyo na yale ya kazi za maendeleo. Hatua hii itaongeza pia gharama za kiinua mgongo na pencheni kwa Serikali na kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

Jawabu la athari hizi ni kwa wafanyakazi nao kujituma zaidi na kwa ufanisi ili kuongeza tija, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kwa ujumla kukuza kwa haraka zaidi uchumi wetu, na hivyo kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia malengo makuu ya Serikali na mustakabali wa Bajeti, kwa mwaka ujao wa fedha, inatarajiwa kuwa katika kila Shilingi inayotumika, senti 58.7 ziende katika Sekta tano zinazobeba malengo makuu ya Serikali ambazo ni Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Elimu na Mafunzo ya Amali, Afya, Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, na Kilimo, Maliasili, Mifugo

na Uvuvi. Kwa ujumla, sekta hizi tano zinatarajiwa kutumia jumla ya TZS 494.2 bilioni kati ya TZS 841.5 bilioni za matumizi ya Serikali yote.

Mhe. Spika, uamuzi huo wa Serikali wa kuelekeza fedha zake nyingi katika sekta hizo una sababu maalum. Kwanza, tunahitaji kuendeleza uwekezaji katika miundombinu yetu ya msingi ili kuwa chachu ya maendeleo yetu ya kiuchumi na kijamii. Asilimia 22.4 ya Bajeti inaelekea katika Sekta hiyo. Pili, huduma za Elimu na Afya nazo pia zina umuhimu wa kipekee katika maendeleo ya wananchi.

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha ongezeko la wanafunzi katika elimu ya msingi kutoka wanafunzi 233,883 mwaka 2014 hadi 239,274 mwaka 2015. Kwa elimu ya Sekondari, idadi hii nayo imeongezeka kutoka wanafunzi 74,868 hadi 79,608. Kwa upande wa afya, takwimu zinaonesha mafanikio kwa mwaka 2015 kwani idadi ya wagonjwa waliotibiwa katika hospitali za Serikali imepungua kutoka 440,201 mwaka 2014 hadi 438,973 mwaka 2015 wakati idadi ya vifo ikipungua kutoka 1,864 hadi 1,700 katika kipindi hicho. Pamoja na mafanikio haya, bado tuna jukumu la kuendelea kuimarisha huduma za jamii na afya ili kuwaondolea wananchi mzigo wa maradhi.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, Serikali inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 482.4 bilioni kutokana na mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2016/17. Kati ya mapato hayo, jumla ya TZS 32.1 bilioni ni mapato ambayo yameanzishwa kisheria na hivyo hayawezi kuingizwa katika mapato ya jumla ya matumizi. Mapato haya ni pamoja na ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu, Mfuko wa Miundombinu, matumizi ya Bodi ya Mapato (*ZRB*) na mapato maalum kwa ajili ya utengenezaji wa madawati. Ukiondoa mapato hayo, Serikali inabaki na TZS 450.3 bilioni.

Mhe. Spika, Serikali pia inakabiliwa na matumizi mengine ya kisheria na ya lazima, ambayo kwa mwaka ujao wa fedha yanatarajiwa kufikia TZS 404.4 bilioni yakihusisha mishahara (pamoja na ruzuku) TZS 251.1 bilioni, matumizi ya lazima ya Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 59.3 bilioni, matumizi kwa Miradi ya Maendeleo TZS 58.0 bilioni, Elimu (Elimu ya Juu, Baraza la Mitihani na gharama kwa Elimu ya Msingi) TZS 19.5 bilioni, Pencheni kwa Wazee TZS 6.5 bilioni, Ununuzi wa Dawa TZS 4.5 bilioni pamoja na matumizi mengine ya lazima ya TZS 5.5 bilioni. Kwa ujumla, baada ya matumizi hayo ya kisheria na lazima Serikali itabaki na TZS 49.4 bilioni tu kutokana na mapato yake ya ndani.

Mhe. Spika, pamoja na mapato ya Msamaha wa Madeni wa TZS 1.3 bilioni, bado kutakuwa na salio la TZS 46.1 bilioni wakati mahitaji yaliyobakia ya matumizi yanahitaji jumla ya TZS 80.4 bilioni, na hivyo kuacha nakisi ya TZS 33.0 bilioni. Inapendekezwa kukopa kiasi hicho cha fedha kutoka ndani ili kuziba nakisi hiyo.

HATUA ZA KUBANA MATUMIZI

Matumizi ya Kawaida

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa mapato na ukuaji wa mahitaji ya matumizi, Serikali inaelewa kuwa haina budi kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na kuimarisha ufanisi katika matumizi. Ni lazima kuhakikisha kuwa fedha zinazotumika zinaleta tija kubwa zaidi. Kwa dhamira hii, ni muhimu kuchukua hatua makhsusi za kukata matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mhe. Spika, tayari Serikali imetoa muongozo wa hatua kadhaa zinazolenga kudhibiti zaidi matumizi. Miongoni mwa maeneo ya hatua hizo ni haya yafuatayo:

- i) Kusitisha safari zote za nje zisizo na tija;
- ii) Kusitisha malipo kwa ajili ya semina, mikutano, warsha na kongamano;
- iii) Kusitisha malipo ya posho kwa watumishi wa umma kwa kazi zinazofanywa ndani ya saa za kazi;
- vi) Kuzuia matumizi kwa chakula kwa viongozi na watumishi wa umma wakiwa kazini;
- vii) Kupiga marufuku fedha za Serikali kutumika kulipia watumishi wa umma kupiga kambi katika hoteli kwa ajili ya kufanya “kazi maalum”;
- viii) Kuelekeza udhibiti katika ununuzi wa vifaa vya kuandikia na mafuta; na
- ix) Kuelekeza udhibiti wa matumizi kwa ajili ya sherehe, maadhimisho na machapisho yasiyo ya lazima.

Kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija zaidi

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa wakati mmoja na hivyo kutawanya sana rasilimali chache na hivyo kuchelewesha kupatikana tija kubwa. Mapendekezo ya Bajeti ya mwaka

2016/17 yamelenga kuanza kutekeleza agizo la Serikali la kuandaa miradi michache yenye tija na ambayo ni kipaumbele kwa huduma za jamii na mageuzi ya kiuchumi.

Kudhibiti gharama kutokana na kuanzishwa Taasisi mpya

Mhe. Spika, Idara nyingi za Serikali zimekuwa zikibadilishwa muundo wake na kuwa Taasisi zenye kujitegemea. Sheria nyingi za Taasisi hizo huhitaji Fungu binafsi (*Vote*) au zenye kuingiziwa fedha kwa njia ya ruzuku. Aghalabu Taasisi hizo huwa na mifumo mipya ya kiutawala, kufanya ajira mpya na kuendesha kwa gharama kubwa zaidi za mishahara kuliko zilizopo katika utumishi wa umma wa kawaida. Serikali itaangalia tena eneo hili na kuzingatia uwezo wa kujitegemea kwa taasisi hizo au umuhimu mkubwa sana wa Taasisi hizo ambao unafanya majukumu yake yasiweze kutekelezeka kiidara. Vyenginevyo, uanzishwaji wa matumizi ya vifungu vipya utaakhirishwa hadi pale hali ya mapato itakaporuhusu.

Matumizi ya kodi ya miundombinu (Infrastructure Tax)

Mhe. Spika, wakati wa kuanzisha Mfuko wa Miundombinu, ilikubalika kuwa asilimia 75 ya Kodi ya Miundombinu iliyoanzishwa mwaka jana itumike kwa madhumuni ya miundombinu na asilimia 25 iliyobakia itumike kwa mifuko mingine kadhaa iliyotajwa katika Sheria mbalimbali. Kutokana na mahitaji makubwa ya miundombinu na dhamira ya Serikali ya kuleta maendeleo ya haraka, inapendekezwa kwamba kodi yote ya miundombinu itumike katika shughuli za uimarishaji wa miundombinu pekee. Matumizi ya mifuko mingine yaendeleo kuwa sehemu ya matumizi mengineyo ya Wizara husika na Mfuko Mkuu wa Hazina kwa wakati wa dharura.

Mhe. Spika, sambamba na pendekezo hilo, inapendekezwa zaidi kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, jumla ya TZS 26.6 bilioni kutoka Mfuko wa Miundombinu zitumike kugharamia miradi ya miundombinu ifuatayo:

- i. Uwekaji wa Kamera za Vifaa vya Ulinzi - TZS 18 bilioni;
- ii. Ujenzi wa barabara za Pemba (Chake - Wete na Ole - Kengeja) – TZS 1.7 bilioni;
- iii. Usambazaji wa Umeme vijijini (kisiwa cha Fundo) – TZS 2.0 bilioni;
- iv. Uimarishaji wa Elimu ya msingi, elimu Mbadala na Amali – TZS 1.6 bilioni;

- v. Mradi wa kilimo cha mpunga cha Umwagiliaji – TZS 400 milioni;
- vi. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji – TZS 140 milioni;
- vii. Mradi wa Kuimarisha ufugaji wa Mazao ya Baharini – TZS 100 milioni;
- i) Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar – TZS 1.0 bilioni;
- ii) Mradi wa “*Business Incubator*” – TZS 400 milioni;
- iii) Mradi wa Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi (*hyperbaric chamber*) – TZS 400 milioni; na
- iv) Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali – TZS 500 milioni.

HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, pamoja na kuzipongeza na kuzishukuru taasisi za ukusanyaji wa mapato, *TRA*, *ZRB* na Wizara mbalimbali, Serikali inaamini kuwa bado kuna fursa ya kukusanya mapato zaidi kutokana na vyanzo vya ndani kuliko kiasi kinachokusanywa sasa. Kwa sababu hii, kwa mwaka ujao wa fedha (2016/17) haipendekezwi kupandisha kodi yoyote katika vianzio vyake vya mapato ya ndani, zaidi ya kurekebisha viwango vya ada mbalimbali vilivyopitwa na wakati. Badala yake, inashauriwa kuendelea na hatua makhsusi za kupanua wigo wa kodi, kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji, na kuongeza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, mkazo huu unaendana na dhamira ya Serikali ya kuwa na Bajeti yenye kujitegemea kwa kupunguza utegemezi wa misaada ya ruzuku kutoka nje kama nilivyoeleza awali. Hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

Uanzishaji na usimamizi wa maeneo maalum ya kikodi (Block Management System)

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) zinafanya kazi kwa pamoja ili kuigawa Zanzibar katika maeneo maalum ya kikodi. Lengo la hatua hii ni:

- i. Kuweza kuwabaini walipa kodi wote wa kila eneo na kuwasajili katika mtandao wa kodi;

- ii. Kubaini fursa zote zilizopo kwa kodi mbalimbali katika kila eneo;
- iii. Kuwezesha mapato yote ya Serikali kutambuliwa na kukusanywa kwa urahisi zaidi; na
- iv. Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji kwa kuhakikisha kuwa Taasisi hizi mbili zinawasajili walipakodi wale wale na hivyo kuwezesha kodi zote kukusanywa.

Mhe. Spika, utaratibu huu unakusudiwa kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa kuimarisha usajili wa wafanyabiashara wote kupitia Mrajis wa Biashara, matumizi ya *TEHAMA*, na wafanyakazi wa *TRA* na *ZRB* kugaiwa maeneo makhsusi (*blocks*) ya kusimamia.

Kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya kodi ya ardhi na majengo (Property Tax)

Mhe. Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Wathamini wa Majengo, ukusanyaji wa Kodi hii unakusudia kuanza rasmi mwaka 2016/17 mara tu utekelezaji wa Sheria hiyo utakapoanza. Kwa kuanzia, kodi hiyo itakusanywa katika majengo yanayotumika kwa biashara.

Kuyafanyia kazi mapendekezo ya kuongeza mapato yaliyoibuliwa katika maabara ya mapato

Mhe. Spika, Utakumbuka kuwa katika Mpango wa “Matokeo kwa Ustawi – *R4P*”, moja ya eneo lililowekewa mikakati ni la utafutaji wa mapato ya ndani. Mikakati hiyo itaendelea kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha.

Kuongeza udhibiti wa misamaha ya Kodi

Mhe. Spika, misamaha ya kodi isiyo na tija inaathiri uwezo wa Serikali kutoa huduma bora zaidi kutokana na kupunguza uwezo wake kifedha wakati ikinufaisha watu wachache. Serikali itaendelea kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi pamoja na kuzuia matumizi mabaya kwa ile misamaha inayotolewa.

Kupambana na magendo ya mafuta

Mhe. Spika, uingizaji wa aina mbalimbali za mafuta ya petroli ni eneo muhimu la mapato ya Serikali. Kuendelea kwa magendo ya mafuta hayo kunaendelea

kuathiri mapato ya Serikali. Hatua zaidi za udhibiti wa magendo hayo zitaendelezwa ikiwemo kudhibiti mauzo ya mafuta nchini, katika vituo rasmi na visivyo rasmi.

Hatua za Kiutawala

Mhe. Spika, kwa upande wa hatua za kiutawala, maeneo yatakayosimamiwa kwa karibu ni pamoja na haya yafuatayo;-

Ada ya Ukaguzi wa Bidhaa katika kituo (Destination Inspection Fee) na Uthibitishaji wa Bidhaa (Customs Declaration-TANSAD)

Mhe. Spika, Idara ya Forodha nchini imekuwa ikitoza ada ya ukaguzi wa bidhaa katika kituo (*Destination Inspection Fee*) kwa asilimia 0.6 ya thamani ya bidhaa iliyoingizwa na Ada ya Uthibitishaji wa Bidhaa (*Customs Declaration-TANSAD*) ambayo ni 10 USD kwa kila kadhia ya Forodha. Mapato kutokana na ada hizi hubakishwa Idara ya Forodha kwa dhamira ya kujengea uwezo na kuleta mageuzi.

Mhe. Spika, ada hizi hazitowzi hapa Zanzibar na kuifanya Idara hiyo kuendelea kusubiri mgao wa Fedha kutoka makao makuu. Inapendekezwa kutoza ada hizo hapa Zanzibar kuanzia tarehe 1 Julai 2016 na kuziweka katika mfuko maalum (*Basket Fund*). Mapato kutoka mfuko huo yatumike katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani nchini kote, ikiwemo uimarishaji wa Idara ya Forodha (*mordenization*), Idara ya Mapato ya Ndani ya *TRA* na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa *ZRB*. Hatua hii inatarajiwa kuingiza jumla ya TZS 6.68 bilioni.

Vibali vya Kodi kwa Wazabuni (Income Tax Clearance Certificate)

Mhe. Spika, Serikali imeendelea kuwa ni mnunuzi mkubwa wa bidhaa na huduma, kupitia zabuni mbalimbali. Kwa bahati mbaya, katika ununuzi huu, baadhi ya Wazabuni wanaofanya biashara na Serikali hawalipi kodi ipasavyo. Muongozo maalum utatolewa kwa kila Wizara, Idara inayojitegemea na Taasisi zote za Serikali zisitoe zabuni kwa wazabuni wasiokuwa na uthibitisho wa kupipa kodi (*Tax Clearance Certificates*) kutoka *ZRB* na *TRA*.

Usajili wa Jina la Biashara (Business Registration Name)

Mhe. Spika, kutokana na kufanana kwa majina ya wafanyabiashara wadogo wadogo kunakopelekea ugumu wa kutambulika katika Taasisi za kodi (*TRA & ZRB*), wafanyabiashara wote nchini watatakiwa kusajili jina la biashara kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya Serikali. Hatua hii itakwenda sambamba na uimarishaji wa usimamizi wa kimaeneo (*Block Management System*) ulioelezwa hapo kabla.

Usimamizi wa mapato kutokana na Ardhi

Mhe. Spika, bado kuna fursa kubwa ya kuongeza mapato kutokana na matumizi ya ardhi. Kumeanza pia kujitokeza miradi mikubwa ya uwekezaji katika ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kukodisha na kuuza (*real estate*). Kwa ujumla, matumizi ya ardhi yanajitokeza kuwa chanzo muhimu sana cha uchumi. Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea na matayarisho maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira yanayokusudia kuhakikisha kuwa uchumi huu unaotumia moja kwa moja ardhi unachangia ipasavyo katika mapato ya Serikali.

Uhaulishaji magari kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara

Mhe. Spika, kumekuwa na biashara kubwa ya uingizaji wa gari nchini na baadae kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara. Kwa sasa pande mbili hizi za Jamhuri ya Muungano zinatumia mifumo tofauti ya uthamini wa kodi za magari unaopelekea gari hizo kutozwa tofauti kubwa ya ushuru na kodi pale zinapohaulishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Kuanzia Julai 2016, Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar itakadiria na kukusanya tofauti yote ya kodi kabla ya gari kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara.

Usajili wa Vyombo vya Moto

Mhe. Spika, suala la usajili la vyombo vya moto sio la Muungano. Kila upande wa Jamhuri una utaratibu wake wa kisheria wa kusajili vyombo hivyo. Kwa sababu hii, ukiacha vyombo vya Serikali, vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar haviruhusiwi kutembea Tanzania Bara kwa namba za Zanzibar. Ili kuleta usawa katika utekelezaji wa Sheria na usajili, kuanzia tarehe 01 Julai 2016, vyombo vya moto vyenye usajili wa Tanzania Bara vitapaswa kusajiliwa upya Zanzibar kama vyombo vyengine vyote vinavyotoka nje ya nchi.

SURA YA BAJETI

Mhe. Spika, kutokana na maelezo ya hapo juu, Sura ya Bajeti ya mwaka 2016/17 inahusisha mapato ya jumla ya TZS 841.5 bilioni, ikiwemo Mapato ya Ndani ya TZS 482.4 bilioni, Mapato kutoka nje ya TZS 324.8 bilioni, fedha kutokana na Misamaha ya Madeni ni TZS 1.3 bilioni na Mikopo ya ndani ya TZS 33.0 bilioni.

Kwa upande wa matumizi, kiasi hicho cha TZS 841.5 bilioni kinatarajiwa kugawanywa kwa TZS 445.6 bilioni kuelekezwa katika matumizi ya kazi za kawaida na TZS 395.9 bilioni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kuwa kati ya fedha zote za TZS 841.5 bilioni, Ruzuku kutoka nje inatarajiwa kufikia TZS 93.3 bilioni tu, hali hii inamaanisha kuendelea kupungua kwa utegemezi wa ruzuku kutoka nje hadi kufikia asilimia 11.1 ya Bajeti ya Serikali, ikimaanisha kupungua zaidi kutoka asilimia 12.2 ya mwaka 2015/16. Hali hii inaashiria kuwa tupo katika njia sahihi ya kupunguza utegemezi kwa utekelezaji wa Bajeti yetu.

MFUMO WA BAJETI 2016/17				
Maelezo	Makisio 2015/16	Matarajio Hadi June 2016	Makisio 2016/17	Ongezeko/ Punguzo la (%)
MAPATO				
A Mapato ya ndani	429.5	391.5	461.4	7.4
B 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	100T	7.7	100T	-
C Kodi ya Mapato kwa W/Kazi wa SMT	21.0	21.0	21.0	0.0
C Dhamana za Hazina na Hati Fungani	30.0	10.0	33.0	10.0
F Msamaha wa Madeni (MDRI)	1.3	0.0	1.3	0.0
G Mikopo na Ruzuku	347.1	84.3	324.8	-6.4
H Mfuko wa Wafadhili (BF)	1.5	1.5	0.0	-
Jumla ya Mapato	830.4	516.0	841.5	1.3
MATUMIZI				
Matumizi ya Kawaida	431.4	399.1	445.6	11.7
i) Mishahara (Wizara)	205.8	196.0	223.7	8.7
ii) Mishahara (Ruzuku)	28.6	30.0	27.4	-4.2
iii) Matumizi Mengineyo (Wizara)	84.3	65.6	80.6	-4.4
iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku)	28.5	23.3	31.6	10.9
v) Mfuko mkuu wa Serikali (CFS)	84.2	84.2	82.3	-2.2
Matumizi ya Maendeleo	399.1	116.9	395.9	-0.8
i) Mchango wa Serikali	51.9	32.6	71.1	37.0
ii) Ruzuku	98.3	44.0	93.3	-5.1
ii) Mikopo	248.9	40.3	231.5	-7.0
Jumla ya matumizi	830.4	516.0	841.5	1.3

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SHUKRANI

Mhe. Spika, matayarisho haya ya mapendekezo ya Bajeti ya Serikali yameshirikisha Taasisi na watu mbali mbali. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote kwa namna moja au nyengine ambao wameshiriki katika kufanikisha mapendekezo haya.

Naomba niwashukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyevidi wa Kamati za Kudumu za Baraza lako hili tukufu kwa kuyapitia mapendekezo haya kwa kina na hatimaye kutoa muongozo wa kamati na kuridhia yawasilishwe katika Baraza hili.

Mhe. Spika, namshukuru pia Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wote kwa kuyapitia mapendekezo ya awali kabla ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi na kufanya marekebishi kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza la Mapinduzi yaliyowezesha Mapendekezo haya kuwasilishwa leo hii hapa Barazani.

Mhe. Spika, shukrani za pekee ni kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiwemo wa Tume ya Mipango kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kipindi kifupi. Niruhusu, kwa niaba yao, niwashukuru sana Bwana Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Juma Hassan Reli, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Bwana Ali Khamis Juma, Naibu Katibu Mkuu – Fedha na Mipango, Bwana Mwitwa Mgeni Mwitwa Kamishna wa Bajeti, Makamishna, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi kubwa iliyofanikisha mapendekezo haya kusomwa hapa leo hii.

Mhe. Spika, kwa nafasi hii pia nampongeza Bi. Mwanahija Almasi Ali kwa kuteuliwa na Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushika wadhifa wa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Namshukuru sana mtangulizi wake Bwana Omar Hassan Omar (*King*) na kumtakia utendaji bora katika nafasi yake mpya.

Mhe. Spika, serikali imeendelea kufanya kazi kwa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa. Naomba kuyashukuru sana kwa mashirikiano na misaada yanayotupatia hasa zikiwemo nchi za Canada, China, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nitambue na kushukuru misaada ya mashirika yafuatayo ambayo nayo tumeendelea kufanya nayo kazi kwa pamoja na karibu zaidi. Mashirika hayo ni pamoja na:-

ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD,

ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO na WSPA. (Makofi)

HITIMISHO

Mhe. Spika, baada ya maelezo ya hapo juu, naomba sasa Baraza lako tukufu liidhinishe mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 yenye mapato ya jumla ya TZS 841.5 bilioni zikiwemo TZS 482.4 bilioni za mapato ya ndani, TZS 324.8 bilioni kutokana na Ruzuku na Mikopo kutoka nje, TZS 1.3 bilioni kutokana na misahama ya madeni (*MDRI*) na TZS 33.0 bilioni za mikopo ya ndani.

Aidha, naliomba Baraza liidhinishe matumizi ya 841.5 bilioni ikiwa ni TZS 445.6 bilioni kwa matumizi ya kawaida na TZS 395.9 bilioni kwa kugharamia Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishaji wake, lakini pia napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutaanza kuichangia hoja hii pamoja na ile ya mipango ambayo aliitoa asubuhi mapema leo siku ya Jumatatu, na bahati nzuri nimeshaanza kupata maombi baadhi ya Waheshimiwa ambao wanaomba kuchangia hiyo hotuba. Kwa hiyo, uchangiaji huo utanza siku ya Jumatatu na tunatoa muda huo ili mpate muda wa kwenda kuvipitia hivi vitabu na kuweza kuchambua na kutafakari ili muweze kuja kutoa michango ambayo itasaidia katika kujenga zaidi na kuimarisha hii bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha ambayo ameitoa hivi punde.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaahirisha naomba nichukue nafasi hii sasa kuwatambua wageni wetu waliofika jioni ya leo ambao wametuunga mkono katika bajeti yetu.

Kwanza kabisa naomba kutambua uwepo wa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi. Baada ya hapo naomba sasa niwatambue Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa ambao wamefika hapa kutuunga mkono. Naomba niwatambue mmoja baada ya mwengine nikianza na Balizi Mdogo wa China ambaye amefika hapa, pia nimtambue Balizi Mdogo wa Msumbuji ambaye naye yupo pamoja nasi, nimtambue pia Mhe. Balizi Mdogo wa India.

Napenda pia kutambua uwepo wa Balizi wa Heshima wa Ujerumani (*Honorable Consul of Germany*), pia naomba nitambue uwepo wa Balizi wa Heshima kutoka Italy (*Honorable Consul of Italy*), naomba nitambue uwepo wa Mwakilishi Mkaazi wa *UNDP* Zanzibar, pia nitambue uwepo wa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *UNFPA*. Naomba pia nitambue uwepo wa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *UNICEF*, pia nitambue uwepo wa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *WHO*, na pia nitambue uwepo wa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *ILO*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, napenda pia kutambua uwepo wa Makatibu Wakuu wote wa wizara mbali mbali za SMZ. Pia napenda kutambua uwepo wa Manaiibu Makatibu Wakuu wa wizara mbali mbali za SMZ ambao wamefika, natambua uwepo wa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, pia natambua uwepo wa Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama. Ahsante.

Hawa nitapenda niwatambue mmoja baada ya mwengine waliopo hapa Kamanda wa Jeshi Nyuki Brigedi Zanzibar, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa Zanzibar, Kamishna wa Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar, Kamanda wa KMKM Zanzibar, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi JKU Zanzibar, Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Kamanda wa Vikosi vya Valantia Zanzibar, bila ya kumsahau Kamanda wa Zima Moto na Uokozi Zanzibar. (*Makofi*)

Napenda pia kutambua uwepo wa Mkurugenzi wa Ofisi ya Zanzibar ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pia nitambue Makamishna, Wakurugenzi, na Wenyeviti wa Taasisi mbali mbali za Serikali ambao wapo. Pia napenda kutambua uwepo wa viongozi wa vyama vya siasa vyote vilivyopo Zanzibar, napenda pia nitambue uwepo wa Wakuu wa Vyuo Vikuu vya hapa Zanzibar, nitambue pia uwepo wa Waandishi wa Habari na wale wote ambao watakuwa wameungana nasi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, sasa labda nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili atoe hoja, naomba nikusikilize Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amewasilisha hotuba yake ya bajeti, na kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanahitaji muda wa kuipitia kwa kina bajeti hii ili wapate fursa ya kuichangia, na kwa kuwa kifungu cha Kanuni 94 (5) kinaruhusu kupata siku mbili za kazi kwa Wajumbe kuweza kuipitia bajeti. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kuliahirisha Baraza lako tukufu ili wajumbe wako wapate nafasi ya kuipitia bajeti hii kwa kina mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi barabara. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, sasa napenda nichukue nafasi hii kuwahoji wale wote ambao wanasema tuahirishe mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha mpaka siku ya Jumatatu naomba pia nitambue uwepo wa Kadhi Mkuu wa Zanzibar nilikuwa nimesahau. *(Makofi)*

Baada ya utambuzi huo sasa naahirisha shughuli zetu mpaka siku ya Jumatatu tarehe 23/05/2016 saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 11:12 jioni Baraza liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu
tarehe 23/05/2016 Saa 3:00 asubuhi)*